

YAKINI

 Nina furaha sana kuwa hapa asubuhi hii na kusikia usia huu, wakati tu nilipokuwa nikija jukwaani. Nasikitika kuchelewa, lakini wale wagonjwa nyuma kule, na magari, kama magari ya wagonjwa, na—na ilinibidi kuwahudumia wale ambao hawangeweza kuingia (unaona?) kabla sijaweza kuingia.

Sasa, sijui kama dada yule ambaye ana yule—yule kijana mdogo, kama hawezi kurudi mchana huu. Nataka kuhubiri jioni hii pia, kama Bwana akipenda. Kama hawezi kurudi kwa ajili ya kuwekwa wakfu wakati huo (hali nimekuwa nikisimama muda mrefu sana wakati huu), vema, mwambie a—anaweza kumleta mtoto sasa. Lakini kama anaweza kurudi huu—huu—usiku wa leo; itakuwa afadhali kidogo kwetu. Lakini acha cho chote awezacho kufanya; vyo vyote itakavyomaanisha. Kwa sababu, kama hawezi kurudi, tutamleta yule kijana mdogo sasa awekwe wakfu. Na sasa, yote haya. . . Wakati ninazungumza, kama yeye anataka kuja sasa na—huu utakuwa ndio wakati. . .

Sasa, usiku wa leo kuna jambo maalumu sana. . . Na—nataka kuzungumzia juu ya somo hilo usiku wa leo, ujumbe wa kinabii wa *Bwana, Huu ndio Wakati?* Kwa hiyo kama Bwana akipenda, nataka kuzungumza juu ya somo hilo usiku wa leo: *Huu Ndio Wakati, Bwana?*—au *Bwana, Huu Ndio Wakati?* hasa. Na kisha nataka kuchukua nafasi hii mbele ya kanisa, ambalo. . . Kumekuwa na mambo mengi yaliyotokea katika siku chache zilizopita yanayoelekeza kwenye ki—kitu kikubwa fulani ambacho sikielewi. Lakini tuna—siku zote tuna. . . Njia za Mungu zinapita ufahamu wa binadamu, kwa hivyo inatupasa kutembea tu kwa imani. Kama mtu ye yote angeweza kumuelezea Mungu, basi haitakuwa lazima tena kuwa na imani, kwa sababu una—unajua basi. Lakini tunaenenda kwa imani.

Na asubuhi hii nilifikiria ningejaribu kuwa tu na ibada ya kawaida ya uinjilisti, kwa sababu. . . Kwa namna fulani nimebadili wazo langu baada ya kuja hapa na kuona wengi sana wamesimama, na wamekuwa wakingoja kwa muda mrefu sana. Kisha usiku wa leo, labda ki—kidogo hapa, na kisha naweza kuendelea na hili ninalotaka kusema.

Kitu kimoja ningependa kutangaza wakati wengi wao wapo pamoja—wengi wenu pamoja, ni jambo ambalo nime—nilijizuia kutangaza kwa majuma kadha yaliyopita; yaani, maombi yenu yamejibiwa kuhusu kesi ya kodi ambayo nilikuwa nayo na serikali. Imekwisha. Na kwa hiyo tu. . . Ime—imekwisha sasa. Kama wengi wenu wanavyoelewa, walichonishitakia ni hundi zile zinazotumwa kwa ajili ya mikutano; hata hivyo,

walijaribu kusema zilikuwa zangu binafsi nje huko nao walitaka wanilipishe dola elfu mia tatu na hamsini na kitu kwa kuwa zilikuwa mali yangu binafsi. Na hazikuwa zangu; zilikuwa kwa ajili ya mikutano. Na kanisa linajua kuhusu hilo; ninyi nyote mnajua kuhusu hilo.

Na mwishowe, wamefikia mahali ambapo... (Nitawapa maelezo machache kuhusu yaliyotokea.) Wamekuwa karibu miaka mitatu hadi mitano hivi (karibu miaka mitano, nakisia), katika kesi hiyo, huku na huko, na tabia, na kila kitu. Lakini ninashukuru sana kwamba hawakuweza kunipata na kosa lo lote, kwa hiyo hawakuweza kunishtakia hilo. Kwa hiyo hawakuwa na kitu cha kushtakia, ila walisema tu, kule kuto—kutokujua kwangu mimi mwenyewe, ninadhani. Kwa kutokujua sana kuhusu sheria, watu waliniitea hundi; nami niliziweka sahihi, na kuziandika jina langu, kuziweka katika shughuli za mikutano. Lakini basi mradi naziandika jina langu, zilikuwa zangu. Unaona? Haidhuru... Kasema, “Hilo ni zuri sana kwako wewe ku—kama hivyo, lakini zilikuwa za kwako, kisha unazitoa kwa kanisa. Lakini mara tu ulipoandika jina lako juu yake, zilikuwa za kwako; haidhuru zilitolewa kwa makusudi gani, ziliandikwa wewe.” Kwa hiyo, na kama zingewekwa katika—mtu fulani angeandika hapo “zawadi ya mtu binafsi,” ingekuwa sawa; lakini waliandika tu “*William Branham*” (unaona?); na wakati nilipoandika jina langu juu yake, ili—hilo liliharibu mambo yote; Hayo tu. Kwa hiyo walikuwa... Na mwishowe kwa maombi...

Na kisha si muda mrefu uliopita, unajua, wao—nilipata ono kwamba jitu kubwa jeusi, lenye moshi, lenye masinzi, lenye magamba (kama mamba), lilinikaribia, lenye vidole vya chuma. Nilikuwa na kisu kimoja kidogo, hivyo, nalo lilikuwa limeandikwa juu yake *Serikali ya Marekani*. Nami sikuweza kufanya jambo lo lote, sikuwa na msaada; na kisha Bwana akajitokeza, nalo lilishindwa. Na mnakumbuka mimi naliwaambia hilo muda mrefu uliopita.

Nao waliomba mapatano hivi majuzi. Na wakili wangu, bwana Orbison huko New Albany, na Ice & Miller huko Indianapolis katika kesi ya kodi waliniita na kuniambia, “Shuka uje!” Basi nilishuka, Ndugu Roberson, pamoja nami, na mke wangu, na wadhamini wa kanisa hapa, na sisi sote; tulienda, nao walituambia kwamba walikuwa—serikali ilikuwa imekubali kupatana.

Nami nalisema, “Mimi—kama nadaiwa cho chote na mtu, nitawalipa. Lakini na—najitahidi sana, lakini,” nilisema, “sidaiwi hizo.” Na kwa hiyo nalisema, “Mimi—mimi—ni... Kwa kweli, Mungu ajua. Na kwa nini basi wasinishtaki kama nina hatia?” Nilisema, “Walikuwa na miaka mitano kujaribu kulifanya, lakini hawakuweza kuona kitu cha kufanyia hilo.”

Kwa hiyo nalisema, “La, Mimi—na hisi sitalipa tu mpaka ikathibitishwe kwamba nadaiwa.”

Na kisha yule wakili aliniingiza ndani na akazungumza nami, akasema, “Sasa twaweza kufanya kesi. Serikali itaifanya.” Na akasema, “Watakapoifanya, kitu pekee wawezacho kupata dhidi yako ilikuwa kwamba wewe. . .”

Kile mimi—kile. . . Namna nilivyolitenda; sikufanya tu. . . Sijui kitu kuhusu uhasibu, kwa hiyo ilinibidi tu nilifanya hilo jinsi nilivyofikiria ndio uaminifu. Na ilikuwa—kamwe haikuwekwa benki kwa jina langu; wakati wote ilikuwa imewekwa katika jina la kanisa, mikutano, na kadhalika. Unaona? Kwa hiyo hakukuwa na kitu ambacho ningeweza kufanya kuhusu hilo.

Na mimi. . . Yeye akasema, “Vema, wanakubali kupatana kwa dola kumi na tano elfu, na dola kumi elfu za faini;” na gharama ya wakili ilikuwa elfu kumi na tano. Hilo lilinigharimu arobaini elfu. Na kwa hivyo basi wanataka tano zaidi, nafikiri ndivyo sasa, kwa hiyo nalikwenda. . . Nikasema, “Naweza kupata dola elfu arobaini wapi ulimwenguni?” Nikasema, “Mwajua akiba yangu ya benki hapa, inasema kama dola mia moja na labda pungufu.” Nalisema, “Nitapata wapi dola arobaini elfu na kitu?” Nami nikasema, sina kitu cha kutegemea; mimi sina tu. Hivyo tu.”

Naye alisema, “Bwana Branham,” akasema, “jambo lenyewe ni hili: Kama tukifanya kesi,” alisema, “hapana shaka, ila tutashinda kesi.” Akasema, “Lakini hapa ni kwa—ile. . . Tunaweza kushinda, kwa sababu nitafanya hivi. Watadai hizo zote ni zako, kwa sababu uliweka sahihi yako katika hizo hundi. Nao wanakwenda kudai ni zako ingawa ziliwekwa benki katika jina la mikutano, kanisa, mikutano ya Branham, na kisha kanisa.”

Na hakuna wakati mmoja waliweza kuona senti moja niliyowahi kutumia mimi mwenyewe. Huo ni ukweli; Mungu ajua! Kuna mtu aketiye papa hapa sasa, amekuwa wakati wote yu pamoja nami. Hapakuwa na senti moja niliyowahi kutumia kwa ajili yangu. Zote zilikuwa kwa Ufalme wa Mungu, kila mahali, kila hundi, kila kitu kingine.

Lakini unaona hilo? Lakini hilo si hoja. Ilikuwa—mimi—ilipaswa iwe yangu kwanza na kisha, ya kanisa, ya mikutano. Na mwajua, wanayo namna ya kulifanya hilo, namna zote za kukwepea wanazoweza kutengeneza. Kwa hivyo basi nilisema, “Vema, mimi, ni—sitafanya hivyo,”

Naye alisema, “Vema, kama tukishinda kesi namna hiyo, kwa sababu nita—nitazitangaza kama zawadi za binafsi.” (Unaona?) Nitaitangaza, kwa serikali, zawadi za binafsi. Naye alisema, “Basi, nifanyapo hilo, zaidi ya dola kumi elfu

zitakuwa urithi; kisha, utakuwa katika tatizo hilo hilo tena, na watakushikilia miaka mitano mingine wakikagua zote.”

Unaona? Unapoandika hundi inapitia afisi ya kuidhinisha hundi; wanaipiga picha, nakala ya hundi hiyo. Bila shaka, nilikuwa pia na hundi zote, ambazo iliziidhinisha.

Kwa hiyo walisema, “Hapo ndipo wanapokurudisha moja kwa moja tena.” Naye alisema, “Kitu kingine, Bwana Branham, kama ukiwahi wakati wo wote kuitwa na serikali, kama hivyo, chini ya uchunguzi, haidhuru ufanye nini, mbele ya macho ya umma wewe ni mjanja.” Unaona? Kasema ni hayo tu.

Angalia huyu mhudumu mdogo wa Kibatisti hapa Mississippi. Maskini mtu huyo... Mwanamke fulani alisema yeye alikuja akamtukana. Na mwanamume huyo alileta mashahidi toka kote nchini na kila mahali (hata hakuwepo mjini kwa masiku kabla ya siku ile au siku iliyofuata), hata ikawa hakimu alitaka kugeuka amuambie amshitaki huyo mwanamke kwa kumkashifu. Alisema, “Mwachilie yeye aende.”

Na wakati hilo lilipotangazwa kwa uchunguzi nchini, unajua nini kilitokea? Asilimia sabini na tano ya Wamarekani walisema “Palipo na moshi, hapakosi moto.” Na maskini huyo jamaa (bila kosa kama ambavyo ningekuwa au mtu mwingine ye yote) atakabiliana na hilo maishani mwake mwote, ingawaje hakuhusika na hilo kabisa.

Niliona vibaya sana, kwa muda, kuwazia kwamba nimetoa maisha yangu kwa Ufalme wa Mungu kujaribu kuwafanya (unaona?) watu walipe kodi zako, na kufanya mambo, na kutenda haki, na kuwafanya waovu wawe watu wazuri, na nimelazimishwa kuwa kana kwamba mimi mwenyewe nilikuwa mjanja.

Nikawaza, “Nimefanya nini duniani?” Na kisha ikanijia, na nikaangalia katika Biblia. Kila mtu katika Biblia, hakuna aliyetengwa kando, ambaye aliwahi kuwa na huduma ya kiroho, kama Shetani hakumnasa katika mambo ya maadili au kitu fulani, serikali iliwakamata. Rudi nyuma po pote unapotaka, wakati wote uliopita—Musa, Danieli, wana wa Kiebrania, Yohana Mbatizaji, Yesu Kristo (aliuwawa na serikali—adhabu ya kunyongwa), Paulo, Petro, Yakobo mkuu, Yakobo mdogo, kila mmoja wao alikufa mkononi mwa serikali, kwa sababu ndivyo ilivyo, kila serikali ni ki—kiti cha Shetani, Yesu alisema hivyo; Biblia husema hivyo. Unaona?

Kila serikali inatawaliwa na ibilisi. Kunakuja serikali ambayo itatawaliwa na Kristo; lakini hiyo ni katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Lakini hii—serikali hizi sasa, haidhuru tunazifikiria kuwa njema jinsi gani, lakini nyuma yake zina—zinatawaliwa na Shetani. “Milki hizi,” alisema, “ni zangu; nami hutenda nazo cho chote nitakacho. Nitakupa zote, kama utanisujudia.”

Yesu alisema, “Nenda zako, Shetani! Nawe utamuabudu Bwana, na Yeye pekee utamtumikia.”

Na kisha nilikata tamaa (mke wangu ananisikiliza); nilikwenda zangu nyumbani nami nikasema, “La, bwana! Mimi—kama ningalidaiwa hizo, ningelizilipa, sidaiwi hizo, nami sitazilipa. Hivyo tu.” Nikasema, “Nitazilipaje basi?”

Kwa hiyo nilikwenda zangu nyumbani nikasema, “Meda, wanawishe watoto uso, tayarisha nguo zao; ninaondoka.” Nikasema, “Wala hawata... Kila kitu kimevurugika.” Nami nikasema “Nimefanya nini? Niambieni!” Na nikasema, “Hata hivyo, eti mimi dola elfu arobaini? Whiu! Hamtambui hilo linamaanisha nini kwangu!” Naye akaja akaingia kama mke mdogo mzuri angeweza kuwa, akasema... Nikasema, “Ninaondoka!”

Akasema, “Wadhani hilo litafaa kitu chochote? Umekwisha lifanyia maombi bado?”

Nikawazia, “Vema, labda ingefaa niombe tena.” Narudi ndani tena, na ilionekana kana kwamba Yeye alinena nami. Andiko. Siku zote tunataka kuangalia Maandiko, yale Mungu alifanya kuhusu hilo. Unaona?

Na siku moja Yeye aliulizwa, unajua, wakijaribu ku—wakijaribu kumshitaki kwa serikali, walisema, “Ni sawa kwetu sisi Wayahudi tulio huru kulipa kodi kwa Kaisari?”

Naye akanena, “Mna dinari?” Kasema, “Ina anwani ya nani?” Kasema “Ni ya Kaisari.”

Kasema “Basi, mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu.”

Nami niliwazia hilo, nilifungua katika Biblia yangu na kuisoma. Nikawaza, “Kweli, Bwana, hilo ni sawa! Lakini hizi si mali ya Kaisari, hizi zilikuwa Zako, hazikuwa za Kaisari. Kama zingelikuwa zangu, na imenilazimu—ilinibidi nilipe kodi zaidi au jambo fulani, vema, hilo lingekuwa tofauti. Hizo—zilikuwa za Kaisari, lakini hizi—hizi ni Zako. (Unaona?) Nazo—hazikuwa kwanza za Kaisari.”

Wajua, siku zote Yeye anajibu katika Neno. Nikaendelea tu kusoma, na akasema, “Aisee, Simoni, huna—huna ndoana ya samaki mfukoni mwako? (Unaona?) Siku zote unachukua kijindoana kidogo na usi. Na ndiyo tu niweke akiba asubuhi hii katika benki ya samaki chini kule katika—katika mto, unajua.” Akasema, “Yeye—niliweka akiba na hakika huyo mweka fedha za benki atatoa alichochacho. Nenda tu huko ukaitupe ndoana mtoni na ufikapo ukingoni, funua kinywa chake (unaona?), naye atatoa sarafu ile. Tusiwakwaze. Usiwakwaze. (Unaona?) Nenda ukalipe, Simoni; hiyo itakuwa kwa ajili Yangu na kwa ajili yako.”

Nikawaza, “Kweli, Mungu, una benki za samaki na kila kitu kingine nchini pote. Sijui itafanyikaje.”

Lakini tulishuka; niliwapata ndugu hapa hapa kanisani ambao walidhamini deni yangu. Nami nikaandika kuhusu hiyo deni, na kupata zile dola arobaini elfu, kisha nikailipa. Nikaenda nyumbani; nikataka nijue namna nilivyoandika hundi ile kama watanjia tena. Nikasema, “Hii ni kusema kwamba nimekuwa huru na kodi zote.”...?...ye yote yule atakayeitokea sahihi hiyo, hakika watakuwa katika matatizo baada ya hayo.

Niliendelea kuwapigia simu benki kuona kama watafanya hilo, na hatimaye Bob aliniambia; alisema, “Billy wamelifanya.”

Nami nikaingia na kumkumbatia mke wangu; nikasema; “Mpenzi, niko huru!”

Jinsi mtu anavyojisikia kuwa huru. Na kwa hiyo ninaweza kuzilipa sasa (walinirahisishia sana), naweza kulipa kwa dola elfu nne kwa mwaka. Sasa, si—siwezi kuzurura tena, jamani; yanibidi kuondoka niende kazini. Kwa hiyo mimi—mimi... Itanichukua miaka kumi kuzirudisha na—kama—kama—Yesu haji. Na wakati huo—wakati ajapo, madeni yote yamekwisha lipwa kwa vyo vyote, mwaona...Kwa hiyo basi...Kwa hiyo natumaini ninyi nyote, mimi...Maombi yenu (na usiku wa leo nitaendelea na kitu kidogo tu kwa hilo), lakini maombi yenu ndiyo yaliyonisaidia. Asanteni sana. Mungu awabariki. Haidhuru tuwe wapi, kamwe sitalisahau hilo.

Usiku wa leo, kama Bwana akipenda, nataka kutaja baadhi ya kweli ambazo ninajua, nanyi hakikisheni mtakuja. Sasa kumbukeni, *Mabwana, ni Wakati Gani?*

Sasa, twaenda ku...Naamini wana ratiba kamili kwa muda wote uliobakia wa—juma hili—na Jumatatu usiku ni—ibada ya leo, na usiku wa leo, na Jumatatu. Jumatatu usiku ni usiku wa ibada ya mkesha. Na—kisha, hilo linakupa Jumanne, siku ya Mwaka Mpya, kama unatoka nje ya mji, unaweza kurudi nyumbani. Nasi tutakuwa na baadhi ya wahudumu wazuri hapa sasa, kwa mkutano huo—sisi—ku—kundi kubwa la wahubiri wazuri. Na kila mtu atakuwa akihubiri kwa zamu na kuendelea hadi usiku wa manane; na wakati mwingine wanashiriki Meza ya Bwana (kama ndivyo ilivyopangwa, sijui kama wamepanga wakati huu au la) wakati wakiwa...Wanapopiga mayowe, na makelele, na kufyatua risasi, kunywa pombe, na kuendelea, sisi tutashiriki Meza ya Bwana (Amina!), kuanza mwaka mpya moja kwa moja na Meza ya Bwana.

Sasa, nyote mmekaribishwa, na natumaini kwamba ninyi—Mungu wa mbinguni atawapeni nafasi ya kubaki kama mkiweza.

Sasa, kabla ya kukaribia Neno, nataka ninene hili pia, kwamba bila shaka ninalishukuru kanisa hili, washiriki wake, kwa suti hii nzuri mliyoinunulia. Asanteni sana. Hilo ni

jambo kuu kwangu: kadi zenu zote na vitu vingine kwa—ma—majira ya Krismasi, na zawadi ambazo mliwapelekea jamaa yangu; na lo, mimi—zilikuwa hazihesabiki kwangu, na mambo madogo madogo ambayo hayawezi kugusa sehemu ile katika moyo wangu. Hakuna kitu kingeweza kufanya jinsi hiyo, kujua kwamba zimetoka kwenu.

Na kwa hiyo, baadhi yao wamenipelekea zawadi zao za Krismasi kifedha, na baadhi yao walipeleka... Kama vile, ndugu mmoja alinipelekea daftari dogo ya mfukoni na—ambayo ameitengeneza na jina langu juu yake; na pini dogo ambapo unaangalilia; na ina Sala ya Bwana ndani yake; na lo, mambo kama hayo, ni jambo tu—tunazithamini sana. Mimi na mke wangu na watoto, twataka kuwaambieni asanteni sana. Ni jambo dogo sana, lakini nitasema hili (hili ndilo neno kuu sana kuliko yote, nafikiri, ambalo mtu ye yote angeweza kusema) “Mungu awabariki.” Hakuna kitu kiwezacho kuwa kikuu zaidi ya hilo.

Sasa, na kwa ndugu hawa hapa kanisani walioninunulia bunduki ile, mimi—mimi nilivaa suti yangu, lakini mimi—mimi sikuweza kuileta ile bunduki kanisani. Lakini ilikuwa... Kwa kweli wangukuwa na kitu dhidi yangu. Sivyo? Kwa hivyo mimi—mimi—mimi nawashukuruni hakika, ndugu zangu. Na nilikuwa niasome majina yao kidogo... Bali mmoja wa hao ndugu alinjia jana; kasema, “Lo, usi—usi—usinishukuru mimi, Ndugu Branham, itaondoa mara moja furaha yote katika hilo.” Unaona?

Kwa hivyo naliwaza, “Labda wengine wao wangeweza kufikiria kitu kile kile.” Lakini nina majina yenu; waliyachapisha. Siku zote nitalikumbuka, na Bwana awabariki sana.

Nanyi mwajua ninapopumzikia, na huenda katika chumba cha faragha, na kuketi, na kuwazia mambo mbali mbali. Ubongo ukijaa nisiweze kuendelea, basi hufikiria safari ya kuwinda niliyoenda mahali fulani, au mahali fulani nilipokwenda kuvua samaki. Nafurahia hayo. Mungu awabariki.

Sasa, twaweza kuinamisha vichwa vyetu kwa kitambo kidogo tunapokaribia Neno! Nina hakika kuna haja hapa asubuhi hii nyingi mno hata hatuwezi kuzihesabu hivi sasa, kwa hivyo sijui, tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, haja zenu maalumu, kama mtazishikilia tu mioyoni mwenu, na kuinua mikono yenu tu na kusema, “Mungu, wajua kile ninachowazia sasa.”

Bwana Yesu, wauona kila mkono; nawe wajua kitu gani kiko nyuma yake. Chini ya mkono huo kuna haja. Nasi twaja sasa, kwa heshima kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu Aliye Hai, lulu ile kubwa nyeupe inayojitandaza katika anga za wakati, anakokaa Mungu Yehova, na damu ya Yesu ikiwa juu

ya madhabahu. Nasi twazungumza kupitia damu hiyo kwa Yeye aliyesema, “Mwombeni Baba jambo lo lote katika Jina Langu; mtapewa.” Je, hutasikiliza, Mungu, asubuhi hii na kujibu maombi yao? Naweka maombi yangu pamoja na yao leo kwamba utatujalia hilo.

Hapa pana vitambaa vilivyowekwa hapa, Bwana, ili kwamba wagonjwa na wanaoteseke... Na tunafundishwa katika Biblia hiyo kwamba walichukuwa toka kwa Mt. Paulo lesi; na vitambaa na viliwekwa juu ya wagonjwa, na roho wachafu waliwatoka, na maradhi yakatoweka. Na Baba, kwa kuwa tumejua kwa muda mrefu, na hakika twajua, kwamba sisi si Mt. Paulo; lakini hata hivyo, twajisikia kwamba haikuwa Mt. Paulo, ilikuwa Kristo ambaye alikuwa ndani yake. Na Wewe ni Yeye yule jana, leo, na hata milele kulingana na Maandiko.

Sasa, watu hawa, Bwana, wanaamini kwamba tukimuomba Mungu, na kuchukua lesi hizi, na kuziweka juu ya wagonjwa wao, kwamba watakuwa wazima. Naomba kwamba itakuwa hivyo, Bwana. Wakati lesi hizi zinawekwa juu ya wagonjwa... Kama ilivyonenwa, wakati mmoja Israeli wakianza kuwa katika huduma, wakienda kwenye nchi ya ahadi na Bahari ya Shamu ikawazuia wakiwa katika huduma, lakini Mungu aliangalia chini kupitia Nguzo ile ya Moto kwa macho ya hasira; na habari ile ikaogopa, nayo ikaondosha mawimbi yake, maji yake; na Israeli waliendelea wakipitia kwenye nchi kavu wakielekea kwenye nchi ya ahadi.

Sasa, Bwana, leo angalia kupitia Damu ya Yesu. Na utaona tendo hili la imani ambalo tunalitenda hapa asubuhi hii; Shetani na aogope na kuondoka; na kila msafiri aliyepo, na kila mmoja ambaye atawekelewa vitambaa hivi, hebu wao—barabara ifunguliwe, ugonjwa uondolewe; na hebu wasafiri kuelekea nchi ya ahadi, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, Nguzo ya Moto. Tujalie, Bwana.

Sasa, bariki ibada, maneno, somo hili, kusoma; Roho Mtakatifu na achukue hilo Neno asubuhi hii na kuligawa kwa utamu kwa kila mmoja wetu, Bwana, tukiwa tunakua kukaribia kitu fulani kikuu, kitu fulani cha ajabu ambacho hatukifahamu. Mioyo yetu inashtushwa kiajabu, Bwana, na tunaomba sasa tunapokaribia kwa kicho na Neno Lako kwamba utatufasiria maana yake. Kwani twaomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa usiku wa leo, msisahau *Ule — Wakati, Ni Wakati Gani?*

Na sasa, asubuhi hii nataka nifungue katika (ninyi mlio na Biblia zenu au mtie alama, kama mkitaka kufanya hivyo)—katika Maandiko, ambako tunataka kuzungumza kwa muda mchache, hupatikana katika Kitabu cha Matendo. Huenda tukasoma sehemu mbili au tatu: Matendo 26:15 kwanza, Matendo sura ya 25 na kuanzia mstari wa 15. Kisha tunataka kusoma Matendo 23:11; na mnaweza kuongezea hili (mkipenda,

labda sitakuwa na muda wa kulisoma) Wafilipi 1:20. Yote ni juu ya jambo lile lile, maneno yale yale.

Sasa, katika Kitabu cha Matendo 26:15, tu—inasomeka hivi:

Nami nikasema, Wewe u nani, Bwana? Bwana akaniambia, Mimi ni Yesu, ambaye wewe unaniudhi.

...inuka usimame kwa miguu yako, maana nimekutokea kwa sababu hii, nikuweke wewe uwe mtumishi na shahidi wa mambo haya uliyoyaona, na mambo ambayo katika hayo nitajidhihirisha kwako;

Nikikuokoa na watu wako, na watu wa Mataifa, . . . ambao nakutuma kwao;

Uwafungue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za Shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na urithi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.

Kwa hiyo, Ee . . . Agripa, sikuyaasi yale maono ya mbinguni:

Bali kwanza niliwahubiria wale wa Damesiki na Yerusalemu, na katika pwani yote ya Uyahudi na wao—watu wa Mataifa, kwamba watubu na kumwelekea Mungu, wakiyatenda matendo yanayopatana na kutubu kwao.

Katika Matendo 23 na mstari wa 11 tena:

Usiku ule Bwana akasimama karibu naye akasema, Uwe na moyo mkuu Paulo: kwa . . . kama ulivyonishuhudia habari zangu Yerusalemu, imekupasa kunishuhudia vivyo hivyo Rumi nako.

Mungu na aongeze baraka zake takatifu kwa kusomwa kwa Neno hili takatifu la neema kuu sana tulilo nalo mbele zetu.

Sasa, nilikuwa nikimsikiliza mtu akizungumza—au akifundisha si muda mrefu uliopita, naye alitumia neno yakini. Nami naliwaza, “Hilo ni neno zuri sana; ninasikia likitumika mara nyingi.” *Kamilifu kabisa.* Hilo ni . . .

Niliangalia katika kamusi, ya Webster. Kulingana na kamusi ya Webster, ni “kamilifu yenyewe; isiyo na mpaka katika uwezo wake; ya kwanza, neno la mwisho.” Na *neni la mwisho* ni “Amina”; hayo tu. *Yakini*, ni—ni “isiyo na mpaka wa uwezo,” neno *yakini*. Ni—ni kamilifu yenyewe. Hayo tu; hiyo yatosha. Nami nilifikiri, “Hicho ni kitu kitukufu; hilo ni neno la ajabu.”

Na sasa, *neni* ni “wazo lililotamkwa.” Kwanza, lazima liwe wazo, kisha linakuwa neno; kwa sababu huneni maneno yako bila kuyawazia.

Tunaponea kwa lugha hatuna wazo; ni Mungu anayechukua yale mawazo; ni mawazo ya Mungu yakitumia

midomo yetu. Hatuwazii au kujua lile unalosema unaponena kwa lugha, kama ni kunena kwa uvuvio. Wakati unapofasiri hujui unalosema; unalinena tu; hayo tu. Unaona? Huyu ni Mungu. Na kutabiri, hutumii mawazo yako mwenyewe; ni Mungu, sababu unasema vitu ambavyo kwa kawaida usingeliwazia kunena. Unaona?

Lakini Neno *yakini* ni uamuzi wa mwisho; na kwa hiyo, nafikiri kwamba kila mtu anapaswa awe na uamuzi wa mwisho. Na kila mafanikio makubwa ambayo yamewahi kupatikana, kumekuwa na yakini nyuma yake. Haidhuru ilikuwa nini, imekuwa na yakini nyuma yake. Na kila mtu ili afanikiwe kitu fulani lazima kwanza awe na yakini. Na huo ndio uamuzi wa mwisho kupitia hili, lile, kurudia *lile jingine*, mpaka unapofikia hiyo yakini au amina au uamuzi wa mwisho wa kile ulicho. . . Inakubidi uwe na kitu cha kushikilia, kwa maneno mengine. Ni nguzo ya mwisho kwa kila ufanisi. . . Iko mahali fulani; yaweza ipitie kwenye mambo mengi tofauti mpaka ifikiapo nguzo ile ya kujishikiza; lakini kuna “amina” kwa hilo lote. Lazima kuwe na kitu kama hicho. Huwezi kuishi bila ya kuwa na moja.

Wewe—ulipooa, hapana budi uliwazia akilini mwako jambo fulani mpaka ukagusa nguzo ile ya kushikilia. Na ilipaswa kuwa upendo kwa mke wako au mumeo. Vema, labda si mzuri kama mke wa Yohana, au yeye, vema—yeye si— *huyu, yule*, lakini ana kitu fulani alichu nacho ambacho wewe—kinakugusa wewe. Wewe—wewe—unasema, “Huenda ikawa si mzuri kama yule mwingine”; au, “huenda ikawa si mzuri kama yule mwingine;” lakini lazima pawe na yakini hapo kwamba mtu huyo ni tofauti. Na hapo ndipo unaposhikilia. Na kama hiyo haipo hapo, afadhali usioe, hiyo nguzo ya kushikilia, hiyo yakini.

Twaweza kufikiria wengi waliokuwa na yakini katika Biblia. Lo, jinsi tungeweza kufuatilia katika mkondo wa hiyo Biblia, na kuendelea kuwepo hapa kwa majuma mawili tangu sasa, na hata tusinguse upande wa juu, kama tungefikiria hizo yakini katika Biblia. Kwa mfano, hebu nitaje moja au mbili, kuwaelezea kifupi.

Mwangelie Ayubu. Sasa, alikuwa na Yakini. Kila kitu kilimuendea vibaya mtu huyo, mtu wa haki. Sasa, tusingethubutu kusema kwamba hakuwa mwenye haki, kwa sababu Mungu alisema alikuwa mwenye haki. Hapakuwa na mtu ulimwenguni kama Ayubu. Alikuwa mkamilifu machoni pa Mungu; naye alijua hilo, kwa sababu alikuwa na Uamuzi wa Mwisho; alikuwa na Yakini.

Wakati kila kitu kilionekana kinyume, maradhi yalitokea, marafiki zake labda wangelisema, “Sasa, ndivyo hivyo, Ayubu, hilo ladhihirisha kwamba unafanya dhambi; umekosea.” Ndiposa, maaskofu walipomjia (waliwaita wafariji wa Ayubu), na badala ya kumfariji, hawakuona kitu ila dhambi katika

maisha yake; kwa sababu Mungu alishughulika naye jinsi alivyofanya.

Na watoto wake waliuwawa; mali ya—yake ilichomwa moto; kila kitu a—a—alichokuwa nacho kilienda kombo, na hata maisha yake mwenyewe yalikuwa katika hatari, akiketi juu ya majivu, majipu yalijaa toka utosini mwake hadi kwenye nyayo za miguu yake. Na hata yule mwenzi wake mpenzi, mzuri, mama wa hao watoto, alisema, “Inakupasa kumlaani Mungu upate kufa.” Lakini usoni mwa hayo yote Ayubu alikuwa na yakini!

Lo, katika wakati wa magonjwa kama tungeweza tu kujifungia kwenye hiyo Yakini. Ayubu alijua kwamba amefanya mapenzi ya Yehova, naye alikuwa na imani katika yale ambayo ameyafanya, kwa sababu Yehova alihitaji hayo. Kama tu twaweza kutenda hilo! Yahova alihitaji kafara ya kuteketezwa kwa ajili ya dhambi yake. Na Ayubu, si kwa ajili yake tu, lakini kwa ajili ya watoto wake, alitoa sadaka ya kuteketeza, na hayo ndiyo tu yote Mungu aliyotaka.

Lo, waweza kusema, “Laiti angelihitaji hayo tu leo.”

Ni machache zaidi ya hayo, ni imani tu katika Neno Lake. Na wewe—kama ukilifanya Neno Lake Yakini yako, waweza—ahadi yo yote ya Mungu katika Biblia, waweza kujifungia nafsi yako kwake. Haidhuru mawimbi yanakupiga vipi, bado umefungiwa. Yakini yako.

Naye alilishikilia, na wafariji wake waliposema, “Umetenda dhambi,” alijua hakutenda dhambi. Alikuwa mwenye haki, kwa sababu alitenda matakwa ya Yehova. Na wakati yeye ni—kila... Yule mtu aliingia na kusema, “Watoto wako wamekufa,” mwingine akaingia akasema, “Ngamia wako wote wameteketewa na moto ulioanguka kutoka mbinguni. . .”

Angalia mabishano waliyokuwa nayo wanyanyasi wake, “Unaona? Moto ulitoka mbinguni. Sasa, Ayubu, hilo linathibitisha. . .”

“Halithibitishi kitu!”

“Sasa, Yeye asingewapiga wanao, Ayubu; wewe ni mtu mwenye haki.”

Lakini Ayubu alisema “Najua kwamba nimefanya kilicho sahihi.” Bado aliendelea kushikilia; alikuwa na kitu ambacho aliweza kukitumainia. Ndicho hicho. Alikuwa ameyakubali; alikuwa ametenda sawa kabisa na yale Mungu alimwambia afanye; naye alikuwa na hakika kabisa. Sawa!

Kisha, alipofikia mahali ambapo Yakini ilishikilia, ndipo hatimaye alianza kusikia kamba ambayo ilikuwa imelegea ikikaza, ikirukaruka kote. Lakini ikaanza kukazika, na Roho akaja juu yake; naye akasimama, akiwa nabii, akasema, “Najua Mtetezi wangu yu hai!” Amina! Unaona? Alikuwa amejikaza kwa ile Yakini yake; alikuwa amewasiliana. Alijua kwamba

alikuwa ametenda yaliyo sahihi, na siku moja ilimbidi ajikaze kwayo. “Najua Mtetezi wangu yu hai, na ya kuwa siku za mwisho atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi na mwili wangu kuharibiwa na mabuu, bado katika mwili nitamwona Mungu,” Ndiposa alijua; basi Yakini yake ikaweka nanga.

Ibrahimu, yakini, akishuka toka Babeli, toka kwenye ule mnara na kule—kuelekea Shinari, na huko nje alilokuwa anaishi kwa muda na baba yake, na labda alikuwa mkulima. Lakini siku moja, nyuma huko msituni mahali fulani labda akichuma matunda, au—au akienda kuuwa mnyama apate kitoweo, na mahali fulani nyuma kule, Mungu alinena naye alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano.

Naye alikuwa—yeye na mkewe, Sara, akiwa na umri wa miaka sitini na mitano hakuwa na mtoto—bila mtoto, hawakuwa na watoto wo wote. Ndipo, Mungu akamwambia, “Utapata mtoto kwa Sara, lakini ili kufanya hivi, yakubidi ujitenge mwenyewe.”

Ahadi za Mungu siku zote zina masharti. Yakubidi kabisa... Haidhuru wewe ni wa kiasili vipi kwa ile ahadi, iko chini ya masharti siku zote. Jinsi tungenimama hapa na kuyapitia Maandiko, mbele nyuma kwa masaa kadha (unaona?), kwamba yale masharti ndiyo yamaanishayo kitu. Waweza kuwa na kiasili utakavyo, lakini ni chini ya masharti kwa ile ahadi, kuchaguliwa tangu awali, na kadhalika.

Angalia! Sasa Ibrahimu, yeye alimwamini Mungu, na ilihesabiwa kwake kuwa haki. Sasa, lingekuwa jambo ba—baya jinsi gani kuukabili u—ulimwengu uliostaarabika, mwanamume miaka sabini na mitano akiwa na mwanamke wa sitini na mitano (nao wameishi pamoja tangu walipokuwa vijana mume na mke, sababu mke alikuwa nusu dadaye) na sasa alitazamia kupata mtoto kwake. Lakini alikuwa na Yakini. Hapakuwepo na kitu kingalimtikisa.

Na wakati mwezi wa kwanza halikutokea Yakini yake ilishikilia, kwa sababu alijua amezungumza na Mungu. Mwezi wa pili, mwaka wa pili, miaka kumi, na kwenye miaka ishirini na mitano baadaye (alipokuwa na miaka mia moja na Sara alikuwa na tisini) Yakini yake bado alishikilia.

Na Biblia ilisema, wakati maelezo ya maisha yake yalipoandikwa, alisema, “Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu akimsifu Mungu.” Kwa sababu gani? Je, uliwahi kufikiria kwa sababu gani? Alikuwa na hakika, bila shaka yo yote, na kitu tu kilichompasa kufanya ilikuwa kujitenga na watu wake. Na Mungu kamwe hakumbariki mpaka alipolitenda hilo. Alimchukuwa babaye; baba yake akafa. Alimchukua Lutu; na wakati—baada ya Lutu kujitenga na Ibrahimu, ndipo Mungu akamjia, akasema, “Sasa, tembea kote nchini.” Utii, ahadi chini ya masharti, siku zote huambatana na Mungu, na Neno Lake.

Sasa, angalia...Tumchukue Musa. Musa, yule—mtoro mtumishi-nabii, ambaye Mungu alikuwa amemwinua na kumueleemisha katika jumba la kifalme la Farao, na—na Musa alitoka na mafunzo yake ya Kitheologia na alikuwa—mtu wa kwanza, akamuua. Kisha kasoro ndogo ya kwanza ikaja, ndipo Musa aliogopa sana. Kwa nini? Hakuwa na Yakini; alikuwa tu na ushuhuda wa mama yake wa kuzaliwa kwake.

Alikuwa mtoto wa ajabu; alikuwa na neno la mama yake kuhusu hilo. Alikuwa na magombo ambayo Mungu alikuwa nayo (labda katika makaratasi mahali fulani waliyoandika, wakasafiri nayo)—kwamba Mungu angewazuru watoto wake. Alijua kwamba wakati ulikuwa umefika, kama tufanyavyo sasa. Twajua jambo fulani liko tayari kutendeka.

Sasa, Musa alijua kwamba wakati ulikuwa umefika, naye alijua kwamba alikuwa amachaguliwa kwa hilo; lakini hakuwa na Yakini. Unaona? Na siku moja huko upande wa nyuma wa jangwa, wakati alipokuwa amepoteza ono, Mungu alimtokea katika kijiti kilichowaka moto, akasema, “Musa, nimeona mateso ya watu wangu; nimesikia mateso yao na kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao wanaowapa adhabu; nami nimekumbuka ahadi Yangu. Nimeshuka ili niwaokoe; sasa, shuka uende Misri.” Lo, jamani!

Kasema—Musa akilalamika, kasema, “Mimi si msemaji; ukombozi wa—wangu si mzuri sana; hawataniamini!”

Akasema, “Ni nini kilicho mkononi mwako?”

Akasema, “Fimbo!”

Akasema, “Itupe chini!” Ikawa nyoka. Kasema, “Nyosha mkono wako, kamshike mkia!” Ikageuka tena kuwa fimbo. Alikuwa akimpa tumaini, thibitisho. Mungu anapotoa Yakini, anatoa thibitisho kwa Yakini hiyo, siku zote.

Kisha Musa, wakati alipokuwa chini kule, naye akatupa chini fimbo mbele ya wale wachawi wa Farao (na wale wachawi wakaja wakatupa zao pia), Musa kamwe hakukimbia na kusema, “Lo, vema, nilikuwa nimekosea, mimi—ilikuwa ujanja mdogo tu wa kiuchawi na labda nilikosea.” Lakini alijua; alikuwa na hakika kwamba amekutana na Mungu; naye akasimama kimya. Hebu tuseme alikuwa ametenda sawa sawa kabisa na yale Mungu alimwambia atende; vile vile Ayubu alitenda sawa sawa kabisa na yale Mungu alimwambia atende; Musa alikuwa amefuata amri Zake. Basi simama kimya uone utukufu wa Mungu!.

Musa alifungiwa kwenye Yakini yake, agizo lake, naye alisimama kimya. Naye alipotenda hivyo, nyoka wake alimeza nyoka wale wengine. Unaona? Alikuwa amefungiwa kwenye ile Yakini. Mungu alisema, “Utakapokuwa umekwisha kuwatoa hao wana, mtaniabudu Mimi tena katika mlima huu.”

Na jinsi adui katika kila njia awezayo atajaribu kukutoa kwenye hiyo Yakini. Papo hapo walipoanza safari kutoka Misri, walikabwa kooni mwa—mwa Bahari ya Shamu—milima kila upande. Wakaja kupita kwenye bonde na hapo ilikuwepo Bahari ya Shamu—hakuna njia ya kukimbilia milimani, hakuna njia ya kukwepea upande *huu*, na jeshi la Farao likija upande *huu*. Ni mahali jinsi gani pa kusimama! Unaona ambavyo ibilisi anakufikisha mahali ambapo hujui la kufanya? Lakini kumbuka, kama umefungiwa kwenye Yakini hiyo, hiyo imeipata. Musa alijua kwamba Mungu alimuahidia ya kwamba “Mtaniabudu katika mlima huu utakapowatoa. Nami nitashuka kwa mkono wako kuwatoa na kuwaweka katika nchi ile nyingine.” Alidumu papo hapo nalo, kisha Mungu alituma upepo wa mashariki na ukayasukuma yale maji kutoka kwenye kina cha bahari, nao walitembea juu ya nchi kavu. Yakini!

Jinsi tungeyapitia Maandiko: Danieli, Yakini yake; Shadraka, Meshaki, na Abednego, Yakini zao; Daudi, Yakini yake. Wote—Yakini!

Paulo alikuwa na moja pia, huyo ambaye tunasoma habari zake. Alikuwa na mwito kiini chake ni Kristo, na hilo ndilo lililokuwa Yakini yake. Hiyo ndiyo sababu hakuwa anaogopeshwa na kile Agripa angesema. Alisimama hapo (na Agripa alikuwa Myahudi, kama tujuavyo)—na hivyo wakati—akiwa amesimama mbele ya hawa wafalme na kadhalika, Mungu alikuwa tayari amekwisha mwambia angesimama pale. Kwa hivyo alikuwa na Yakini, kwa hiyo alikwisha kusimulia sawa sawa lile ono la mbinguni. Alisema, “Mimi si... sikulidharau. Nilikuwa—sikulielewa vibaya, sikukosa adabu mimi mwenyewe.” Lakini alilishikilia naye hakuliasi; alilitekeleza lote kabisa, kwani lilikuwa Yakini. Na maisha yo yote ambayo kiini chake ni Kristo, hayo ndiyo Yakini yako.

Sasa, tangu kukutana Naye uso kwa uso njiani akielekea Dameski, hiyo ilikuwa—ilimaanisha mengi sana kwa Paulo. Sasa kumbuka, mwanzoni alikuwa mwanachuoni; alikuwa mtu mkuu katika Maandiko, lakini hakuwa na nguzo ya kushikilia ila lile baraza la wazee ambalo lilimuunga mkono, na—na hati ya cheo kutoka kwa mwa—mwalimu mkuu. Alikuwa mtu mkuu katika fani yake, lakini alikuwa na mashaka. Kitu pekee alichokuwa nacho, yakini yake ingekuwa yenye nguvu tu kama dhehebu lake lilivyokuwa; hiyo ndiyo nguvu angelipata. Naye alikuwa akilishughulikia kwa uaminifu, naye alikuwa akiwachukua Wakristo, na kuwafunga, na kuwaudhi, na hata alimpiga Stefano kwa mawe.

Nafikiri baadaye katika maisha yake, sababu ya yeye kwenda Yerusalemu, nabii alipomwambia, “Usipande kwenda huko, Paulo, kwani minyororo na kifungo vinakungojea,”...

Kisha Paulo alisema, “Najua hilo; lakini siendi tu Yerusalemu kama shahidi, lakini naenda huko; nami niko tayari kufa kwa ajili ya Yesu Kristo,” kwani alijua lile ambalo amefanya, na hamu yake ilikuwa kutia muhuri ushuhuda wake kwa damu yake—kufa mfia imani, kwa sababu alimuua mmojawapo wa wafia imani wa Mungu.

Na sasa, alikuwa akienda zake Dameski na elimu yake yote (aliketiki chini ya mwalimu mkuu, Gamalieli, na jinsi amefundishwa katika dini yote ya Kiyahudi) hata hivyo pamoja na hayo yote, alikuwa mdhaifu sana, naye hakuwa na uwezo wa kufanya mambo fulani. Na mara, ikatokea Nuru na mlio labda wa ngurumo, kisha akapigwa na kuanguka chini. Naye—alipotazama juu, kulikuwa na Nuru iliyong’aa ambayo ilimpofusha macho. Na hilo lilikuwa jambo la ajabu jinsi gani!

Hakuna mtu mwingine aliyeona Nuru ile, Sauli tu. Ilikuwa ha—halisi sana kwake, hata ikampofusha macho, hangeweza kuona, kipofu kabisa kwa Nguzo ya Moto ikimwangazia moja kwa moja kwa nguvu usoni. Naye alisikia Sauti ikisema, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Akasema, “Bwana, Wewe ni nani?”

Akasema, “Mimi ni Yesu; na ni vigumu kwako kuipiga mateke hii michokoo. Inuka sasa, uende Dameski, na huko utapelekewa na mtu.”

Kisha, alipoinuka toka hapo (na palikuwako mmoja, nabii, huko mjini ambaye aliona katika maono, alipokuwa akiomba, naye akaja), Anania alikuja akaingia alipokuwa Sauli, akaweza mikono yake juu yake, naye aliponywa kwa uponyaji wa Kiungu. Akainuka basi, akabatizwa akiosha dhambi zake, akiliitia Jina la Bwana; ndipo akapata Yakini. Hakuwa mtu yule yule baada ya hayo. Alikwenda moja kwa moja kanisa kwa kanisa, mahali kwa mahali, akijaribu kujenga kile alikuwa amejaribu kubomoa.

Jinsi taifa, jinsi ulimwengu wa Kikristo asubuhi hii unavyohitaji Yakini ya aina hiyo. Wale ambao wanachukuliana na kanuni za imani na mapokeo wamejaribu ku—kwa fundisho la mwanadamu, kulipuuzi Neno la Mungu kuwa lile jana leo na hata milele. Wanahitaji Yakini, tukio la kukutana katika barabara ya Dameski, na Mungu Aliye Hai ambaye anaweza kuponya wagonjwa, na kufufua wafu, na kutoa pepo—Yakini halisi.

Paulo alijua kwamba kitu fulani kimetokea; hakuna mtu angalimnyanganya hilo. Hakujali lingine; alikuwa amefungiwa, na hilo lilitosha. Hata ije nini, alijua amefungwa—maisha kiini chake ni Kristo! Lo, maisha aliyokuwa ameishi yalikuwa maisha tofauti.

Sasa kumbuka, alikuwa mtu wa dini. Na kwa baadhi yenu ninyi watu asubuhi hii (na najua mnatambua kwamba kanda hii inanaswa, itasikilizwa na kila taifa chini ya mbingu, karibu

hivyo, kote duniani); na baadhi yenu ninyi watu ambao mpo hapa, sasa; na baadhi yenu nje huko ambako kanda zitasikilizwa katika mataifa mengine kwa mkalimani (akiwapa makabila ya Africa, kule nyuma kwa Wahotentoti, na—na katika—kila mahali); na kwenu ninyi viongozi wa dini ambao mmepata elimu tu ya Biblia (mmeipata toka kwa msimamo wa historia na mwaweza kuelezea mambo yote haya); lakini, kama hamna Yakini, hamna tu—tukio (na kama tukio hilo ambalo—ambalo unadai unalo linakufanya ukane ya kwamba kila moja la neno la hii si kweli kwa kanisa kama ilivyokuwa daima) na unatumainia Shahada yako ya Sanaa, au yo yote uliyo nayo; kama unatumainia mawazo ya dhehebu lako (ambayo yangesema, “Siku za miujiza zimepita; na hatuna uponyaji wa Kiungu, na ubatizo wa Roho Mtakatifu kama walivyopokea siku ya Pentekoste si wa watu siku hizi”); kama hicho ndicho tu ulicho nacho ndugu yangu wa thamani, dada, unahitaji lile tukio la barabara ya Dameski!

Unahitaji kukutana na Mungu huyu Aliye Hai ambapo u—si wazo tu la kubuniwa bongoni mwako, si mtetemeko fulani, au namna fulani ya msisimko, lakini fundisho na tukio dhahiri na la kweli. . . Yesu yule yule ambaye alitembea katika Galilaya anaishi leo na yu hai milele na milele, naye ni yeye yule jana, leo na hata milele—Yakini, ambayo hata si lazima uchukue yale mtu ye yote aliyosema, unajua wewe mwenyewe, si mshtuko fulani.

Na kama mshtuko ambao umeupata—na kama mtu fulani (huenda ikawa ni mshituko wa kweli wa Biblia)—na mtu fulani amejaribu kulielezea vingine, akisema mambo hayo ni ya wakati uliopita, tahadhari! Ni kweli, tahadhari! Lakini kuna njia ya kufahamu. Ijaribu kwa Neno; Hiyo ndiyo Ramani!

Kama nyumba inakwenda kinyume cha ramani, kondrakta ataibomoa na kuijenga tena. Lakini inapaswa iambatane na ramani.

Haidhuru tukio lako ni gani basi, kama kitu fulani ndani yako kinakuambia Biblia hiyo si kweli, kwamba uwezo wa Mungu, mitume, manabii, na waalimu, na wachungaji, na matunda ya Roho si yale yale kama ilivyokuwa wakati alipowamiminikia mitume katika Pentekoste kuna kasoro katika yakini yako; hapana budi imefungiwa kwenye kanuni ya imani ya kidhehebu, badala ya kufungiwa kwa Biblia ya Mungu, aliposema, “Mbingu na nchi pia zitapita, lakini Neno Langu halitashindwa.”

Angalia yakini yako ni nini. Unaweza kuwa na hakika kabisa kwamba una ushirika mzuri na mchungaji, na waweza kuwa na hakika kwamba uko katika ushirika na mzee wa wilaya; na unaweza kuwa na hakika kabisa kwamba una ushirika na askofu, au baadhi ya watu wakuu katika kanisa lako, lakini kama wewe si—Yakini yako si Yesu Kristo. . . “Kwani juu ya

Mwamba huu nitaweka Yakini Yangu, na milango ya kuzimu haitalishinda”—ufunuo wa kiroho wa Yeye ni nani na kumjua Yeye. Sawa!

Lo, sasa, unapokuwa kama Paulo, una Yakini ile ile ambayo alikuwa nayo... Maisha ambayo kiini chake ni Kristo ni maisha tofauti na uliyokuwa nayo kwanza; na huenda ikawa ni maisha ya kidini sana unayoishi.

Lo, nimesikia watu wakisema, “Sasa, wao ni wa kidini sana.” Hilo halina hata uhusiano nalo! Nimekwisha ona tayari dini nyingi, zilizojitolea sana, aminifu mara nyingi sana kuliko wanavyokiri Wakristo wa siku hizi.

Wakati mama unapoweza kuchukua mtoto wake mdogo na, mweusi (mrefu *hivi*) na kumtupa katika kinywa cha mamba, kwa upendo wa mungu wake, nashangaa jinsi Ukristo ulivyo mwaminifu. Wakati mtu anapoweza kujiadhibu sana, angeweza ndoana elfu katika mwili wake, hivyo (ziking’ing’inia na mipira ya maji, zikimshikilia chini hivyo) na kupitia katika mwali wa moto, kutoka hapa hadi mwisho wa maskani yale na (kurejea, nao ukiwa mweupe kwa joto, ukipepewa hivyo), kwa kafara ya mungu wake (sanamu pale yenye macho ya kito chekundu na kadhalika), nashangaa Ukristo uko wapi. Kwa hiyo usifikirie *uaminifu*, uaminifu sio. Uaminifu ni sawa kama ukiwekwa katika kitu sahihi.

Kama daktari akitoa dawa, angeweza kukupa sumu iitwayo aseniki, kwa uaminifu; na angeweza kukupa sumu ya salfiuriki kwa uaminifu; unaweza kujaziwa vibaya kadi ya dawa iliyoamriwa, nawe waweza kuinywa katika uaminifu, lakini hiyo haiokoi maisha yako. Unaona? La, hasha bwana! Yakubidi kujua ufanyacho. Na kitu cho chote kinyume cha Neno la Mungu, sijali ni kitu gani na kimedumu kwa muda gani, bado ni makosa.

Petro aliwapa maagizo ya milele siku ya Pentekoste. Alisema, “Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwani maagizo haya ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Hilo ni sahihi! Ni Amri ya Milele ya daktari.

Sasa, daktari muuza dawa haramu angeliweza kuipata na kukua. Unaona? Bila shaka! Unajua kuna kiasi fulani cha sumu katika amri ya daktari ya dawa kutia sumu kwa kiini cha ugonjwa, na da—daktari anajua tu ni kiasi gani kinachoweza—mwili wako unachokimudu. Kama umezidisha sumu, ingekuua. Na kama huna ya kutosha, basi itafanyika nini? Haitakufaidi kitu kuinywa dawa ile. Anajua kiasi ambacho mwili wako unaweza kumudu.

Sasa, na hivyo ndivyo yalivyo maagizo ya Mungu. Haidhuru mtu mwingine atasema inapaswa kutendwa *hivi*

ama *vile*, usiamini hilo. Unapofuata Neno lile sawa sawa kama lilivyoandikwa, ndivyo inavyotakiwa. Hilo ni sawa! Lishikilie.

Sasa, tuna ile—wale ambao wanasema yakubidi unyunyiziwe. Wana wale wanaosema lazima utumie vyeo vya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; hakuna mambo kama hayo katika Biblia, hakuna mahali kama hapo mtu alipowahi kubatizwa katika Biblia namna nyingine ila kwa Jina la Yesu Kristo. Hilo ni fundisho la sharti ambalo liliongezwa katika kanisa la Katoliki la Kirumi na limeendelezwa kwa mapokeo. (Tutaligusia hilo usiku huu.)

Lakini angalia, katikati ya hayo yote, agizo lile linadumu. Hiyo ndiyo sababu tuna watoto wengi wagonjwa, kwa sababu hawasikilizi ambalo Daktari alisema. Ile Yakini, utakapokuwa umejifungia kwa Hiyo, ndiyo hiyo; Hilo ni Neno la Mungu; haliwezi kushindwa. Maisha yaliyowekwa katika Kristo, ya kidini sana, lakini hayakuwa maisha kiini chake ni Kristo; wengi wetu wana hayo leo.

Nawe upatapo maisha haya ambayo kiini chake ni Kristo, inakufanya wewe ufanye mambo ambayo usingefanya kwa kawaida. Inakufanya uenende kinyume cha ambavyo ungeenenda kwa kawaida. Simaanishi kutenda kipumbavu; ninamaanisha kutenda katika Roho, kitu ambacho ni cha kweli; kitu ambacho ni halisi. Na unapomwona mtu akitenda kipumbavu, unajua wanajifanya tu. Wanajaribu kuigiza hicho kitu halisi kilipo.

Unapoona dola ya bandia, kumbuka kuna dola nzuri ambayo imeigizwa. Unaona? Unapoona ya bandia ni mfano halisi wa kitu ambacho ni cha kweli, ni kitu ambacho—ambacho ni halisi kilichoigizwa.

Angalia, inakufanya ufanye mambo ambayo usingalitenda kwa kawaida. Lo, hicho—ni kitu fulani...Una hakika, una hakika sana nacho unapopata hii Yakini; una hakika yake. Huchukui kilicho—tukio la mtu mwingine. Hiyo ndiyo sababu Ukristo umekuwa kama watoto wadogo katika Biblia na si (samahani)—watoto wadogo shuleni. Wanajaribu kumnakili mwingine; na kama jamaa huyo amkosea, jambo lote ni kosa. Unaona? Kundi lote zima litakuwa makosani. Lo, jamani, usiigize; kutana naye wewe mwenyewe.

Rafiki msiri wangu, akisimama nyuma kule, ni mzee—ni mwana wa rafiki msiri wangu, rafiki wa maisha, maskini Jim Poole. Vema, mimi na baba yake tulikuwa—tumekulia pamoja shuleni, na lo, ni mtu mzuri sana. Mimi na maskini Jim huomba bila kukoma ya kwamba Jim Poole mkubwa awe Mkristo, mwamini wa kweli. Nami na maskini Jim Poole tulikuwa tukizungumza jana kuhusu ambapo tulikutana na Mungu msituni na kumuona katika maumbile. Huko ndiko

unakokutana naye, kwa sababu Yeye ni Muumba, na Yeye yuko katika uumbaji Wake.

Nami nakumbuka, mimi na Jim tulikuwa tukienda—kwenda— tunataka kwenda kuwinda. Na usiku ulipofika, naam, tulikuwa tukienda huko kuchukua baiskeli zetu, na kuzipanda tukipita katika barabara hapa (tukiogopa sana kupitia makaburini baada ya usiku kuanza kuingia), na kwenda huko, na kujinunulia barafu.

Na Jim anapenda kucheza mchezo wa kugonga tufe. Sasa, wakati huo tulikuwa wavulana wa umri wa miaka kumi, kumi na miwili, kumi na minne. Na basi, Jim alipendelea kuketi na kusoma vitabu vya hadithi za kuwinda na kutega mitego. Nami niliketi na kuvuka katika mawazo mengi (unaona?) kuhusu... Na sasa, baadhi ya wavulana wanaweza kuniona. Nami ningeaonaji kibanda mahali fulani, nami nilikuwa na mazoea ya kusema, “Jamani, kibanda hicho kingekuwa kizuri kuwa nacho mlimani.” Na siku zote niliwazia kwamba siku moja nitajijengea kibanda huko milimani, kundi kubwa la mbwa wa kuwindia, na—na bunduki kiasi fulani. Siku zote nalifikiria, “Laiti ningalipata bunduki ya 30-30 wakati fulani maishani mwangu...” Nikafikiri, “Ningewezaje ulimwenguni kupata hata bunduki dogo ya 30-30?” Na hivi majuzi huku nimesimama, nikiangalia ukutani mwangu, na kuona hapo baadhi ya bunduki nzuri sana ambazo zaweza kupatikana, nikawazia, “Neema ya ajabu!” Nilifikiria, “Nitajifunza kupiga shabaha, na kupiga vizuri. Kisha, labda wakati fulani kupata—kufanya safari ya kwenda milimani, mwindaji fulani mzuri atanipeleka kuwa tu namna fulani ya (sababu atapenda kulinda uhai wake labda kutokana na dubu ashambuliaye; hakuwa na hakika sana, mtu fulani tajiri)—angenichukua, kwenda tu naye, namna fulani ya mlinzi. Labda siku moja nitawinda huko Afrika kama mlinzi wa mtu. Kama ningeweza kujifunza.” Hicho ndicho kitu pekee niwezacho kufanya ni kujifunza kuwa hodari, mpigaji shabaha stadi. “Lo,” na naliwaza, “Mungu, wazia hilo, unijalie niwinde kila mahali ulimwenguni. Ni jambo la ajabu jinsi gani!”

Jim alizoea kuketi na kusoma kitabu

Nami nikasema, “Jim...”

Akasema, “Ni—ni—ningependa kusoma kuhusu hilo.”

Nikasema, “Jim, hilo ni lile ambalo mtu mwingine aliisha fanya; nataka kufanya hilo mimi mwenyewe; nataka tukio!” Nilipokuja kwa Kristo singeweza kuchukua tukio la mtu mwingine, nililitaka mimi mwenyewe.

Nakumbuka niliposoma kitabu cha *Mlinzi Mpweke wa Nyota* kilichoandikwa na Zane Grey. Nilikata vifagio viwili au vitatu vya mama, nikiendesha kote nyumbani na kurukaruka, nilipokuwa nimempanda farasi huyu bandia wa fagio. Ni—

nilisoma hadithi hiyo ya—ya mlinzi mpweke wa nyota za mbali, na jinsi ambavyo alileta haki kwa Big Bend.

Kisha nilisoma hadithi ya kubuni ya Edgar Rice Burroughs iitwayo *Tarzan na Nyani*. Mama alikuwa na zulia la sufu, la ngozi ya mnyama wa baharini au kitu fulani ambacho bibi Wathen alimpa toka kwenye moto. Nalo lilikuwa limetandikwa chumbani mwake, nami na—na—nalichukua tu zulia lile nikatoka nalo nje (Mama hakujua upepo haukulipeperusha ukalitoa nje), na nikalitoa nje, na kulikata-kata, na kujitengenezea suti ya Tarzan, na kuketi juu ya mti. Mimi—naliishi nusu ya muda wangu mtini, nje katika suti hii ya Tarzan. Kwa sababu nilikuwa nimeona alilofanya, nilitaka kulifanya pia.

Lakini siku moja kwa neema ya Mungu nilishika kitabu kilicho halisi, Biblia. Wimbo wangu na hadithi imekuwa: “Kuwa kama Yesu; duniani natamani kuwa kama Yeye.” Sitaki kuwa askofu, au—mtu fulani mkuu kanisani, papa fulani, au kasisi fulani. Nataka kuwa kama Yesu.

Ile Yakini, inakufanya tofauti. Kuna kitu fulani katika kulisoma Neno Lake na... Kitu fulani katika moyo wako kwamba unataka kuwa kama Yeye. Una hakika... Ni kama...

Yakini kwa Kristo—Yakini kwa Mkristo ni kama ile—ni—ni kama nanga katika meli. Ndio, wewe—inakubidi kuwa na yakini. Na kama Kristo ndiye Yakini yako, ni kama ile nanga ambayo wakati u... Bahari imechafuka sana, meli inakaribia kuzama, na wewe—tumaini pekee ulilo nalo ni kutia nanga. Kisha, kama meli inayumbayumba (unaona?) kama—nanga ile itashikilia hiyo meli. Mwajua tuna wimbo (ninasahau jina la yule mwandishi sasa, lakini...): *Nanga Yangu Hushikilia*.

Kama yule mvulana mdogo (kama tulivyofikiria mara nyingi) akirusha tiara, hungeweza kuona kitu cho chote, lakini alikuwa na ile kamba. Na mwanamume mmoja alipita karibu akasema, “Unafanya nini, mwanangu?”

Akasema, “Ninarusha tiara yangu.”

Akasema “Una nini mkononi mwako?”

Akasema, “Uzi!”

Kasema, “Hiyo tiara iko wapi?” Akasema, “Siioni. Vema, wajuaje unarusha tiara?”

Akasema, “Ninaihisi; inavuta.” Unaona? Mwishoni mwa uzi ule kulikuwa na yakini. Kwa njia yake ndogo, tiara hiyo ilikuwa yakini yake, kwa hiyo aliweza kusema alikuwa akirusha tiara; ingawa hangeweza kuona, lakini alikuwa ameshikilia kitu ambacho—alikishikilia! Hivyo ndivyo ilivyo mtu azaliwapo mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, ameshikilia kitu fulani ambacho kina nanga nje huko; nayo mawimbi hayamtikisi. Anajua yuko sawa; ametia nanga. Sawa!

Sasa, kama tumo katika mashua yetu dogo, tukielekea kuvuka bahari taratibu ya maisha...Kama yule mshairi mashuhuri alivyosema kwamba:

“Maisha si ndoto tupu!”
Na nafsi imekufa ilalayo usingizi,
Na mambo hayapo kama yanavyoonekana.
Maisha ni sahihi! Na maisha ni amana!
Na kaburi lake sio kikomo chake;
“Kwani wewe ni mavumbi, mavumbini
utarudi,”
Haikunenwa kuhusu nafsi.

Lo, nafikiri hilo ni zuri sana. Sasa, Longfellow aliandika hiyo *Zaburi ya Maisha*. Unaona?

Unaposafiri katika taratibu ya bahari ya
maisha,
Upatapo ukiwa na kuharibikiwa na meli
ndugu,
Unapoona hayo, utajipa moyo. (Unaona?)

Sasa, tumepanda meli, tukiabiri katika bahari taratibu ya maisha; na Kristo, kwa meli juu ya mawimbi ya wakati... Wakati mawimbi yanakuwa makubwa na yanatoswa huku na huko, ninafurahi nina Nanga inayoshikilia katika bonde kule ng'ambo, mahali fulani, hata kifo chenyewe hakiwezi kukuondoa kutoka Kwake. Umefungiwa kwenye Yakini yako.

Kristo ndiye Nanga yetu. Yeye ni Nini? Yeye ni Neno.

*Hapo mwanzo kulikuweco Neno, naye Neno alikuwa
kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*

Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu, . . .

Basi tunapojua kwamba matendo yetu ni sawa kabisa na Neno, tunajua mafundisho yetu yamelingana kikamilifu na Neno (kutoongeza cho chote au kuondoa cho chote, Neno tu); na tunaona matokeo yale yale (kwamba wengine waliotia nanga kwa Neno lile lile) yakiishi katika maishi yetu, basi nanga yako inashikilia. Uhai wa Kristo unajitokeza karibu sana katika njia ya kufanyika mwili kupitia kwako kama ilivyokuwa kwa Kristo, kwa sababu ilikuwa Mungu katika Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. . . Na unamuona Mungu ndani yako mwenyewe akishikilia mkuku uo huo katika Neno, sawa sawa tu na vile Yesu alivyofanya, nawe unaona maisha yake. . .

“Kazi nizifanyazo mimi ninyi nanyi mtazifanya. Yeye aaminiye (si yeye ambaye *anayejifanya anaamini*, yeye ambaye *anafikiri anaamini*, lakini yeye aaminiye)—yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Kwa sababu gani? Ametia nanga kwenye Mwamba ule ule. Je, Mwamba ule ulikuwa nini? Lile Neno, siku zote! Umetiwa nanga hapo.

Ni Nyota yako ya Kaskazini unapopotea baharini. Unajua, tuna nyota nyingi, lakini kuna nyota moja tu ya kweli, nayo haisogei; hiyo ni Nyota ya Kaskazini, sababu imekaa katikati ya dunia. Haidhuru hata kama uko upande wa nyuma, juu chini, po pote ulipo, Nyota hiyo ya Kaskazini iko vile vile. Ni nyota yako ya Kaskazini.

Sasa, unaona? Kuna nyota nyingi sana ambazo husogea toka mahali hadi mahali. Lakini kama uko katika—katika bahari, kwani, baharia ye yote anajua, au mwindaji ye yote anayezurura msituni, anajua kwamba Nyota yako ya Kaskazini ni—ni mahali pako; hivyo tu. Basi, ni kama di—di—dira yako. Dira yako haitalenga kuelekea Mars, au Jupiter, au mahali fulani; itaelekea kwenye Nyota ya Kaskazini. Kwa nini? Hiyo ndiyo yakini yako.

Lo, jamani! Angalia, yakini yako. Lo, nitasema kitu fulani; ninakihisi tu kikija. Angalia! (Najisikia kitawa sana wakati huu, kwa sababu hii ndiyo dhamana.) Angalia! Dira yako yaweza tu kulenga Nyota ya Kaskazini. Hapo ndipo mahali pekee inakoweza kuelekeza. Kama ni dira ya kweli italenga Nyota ya Kaskazini kila wakati. Hiyo ni kweli? Basi kama una Roho Mtakatifu, anaweza tu kuelekeza kwenye Neno! Kamwe hataelekeza kwenye dhehebu; kamwe hataelekeza kwenye kanuni ya imani; kamwe hataelekeza mahali fulani, ataelekeza moja kwa moja kwenye Neno! (Najisikia kupaza sauti!).

Angalia, ni—ni kitu kilicho ndani ya mtu, kikipigapiga. Unapoona Nyota yako imesimama kule, Yesu Kristo, lile Neno; nawe waona Roho yule ambaye yumo ndani yako hataliachia lisogee kulia au kushoto. Huyu ndiye Mmoja wa pekee ambaye anaweza. . . Amekuja kuchukua mambo ya Mungu na kuyaonyesha, kuyadhihirisha.

Na Yesu alisema, “Atatenda tu mambo yale nisemayo hasa. Atawafunulieni mambo jayayo (kuwaonyesha kabla ya wakati wake, kabla ya kufika hapa. Unaona?). Atachukua mambo yale ambayo ni Yangu naye atawaonyesheni. Ndiposa, atawaonyesha mambo yajayo.” (Yohana 15)

Tunaona kwamba anaonyesha mambo; naye anayachukua mambo yaliyo ya Mungu na atawaonyesheni; na atawafunulia mambo ambayo Yesu alisema. Kwa maneno mengine, atayaweka mambo wazi. (Weka hilo kule katika kona usiku wa leo; sababu hilo ndilo tuendalo kutumia muda mfupi ujao.) Akihakikisha, akifanya hilo kweli (unaona?), basi unajua kama wewe—Nyota yako ya Kaskazini, ambayo ni Neno kwa kila Mkristo. . . Kitu cho chote kinyume cha Neno. . .

Tazama! Hebu niwaambieni jambo fulani. Sikilizeni hili kwa makini. Huu ndio ufunuo kamili wa Kiungu wa Mungu, mapenzi Yake, na kuja Kwake Kristo, na kila kitu kimo mumu humu katika Kitabu hiki kimekamilika. Na kama cho chote kinakuondoa kutoka kwa Kitabu hicho, tupilia mbali dira

hiyo, sababu ni kanuni ya imani tu, ni dhehe—ni karatasi tu unayobeba mfukoni mwako, inayoning'inia chumbani mwako imetiwa fremu; ni kanuni ya imani! Jamani, tafuta dira ambayo hukuelekeza kwenye Neno! Amina!

Unaona, ujuzi huu ulipomwangukia Paulo, alikwenda huko Misri na Arabuni mahali fulani na akajifunza miaka mitatu. Utukufu! Ilimbidi awe na uhakika. Naye alipoona, wakati Roho Mtakatifu alipomwongoza neno kwa neno, yeye angeandika hicho kitabu cha Waebrania na kuwaonyesha wale Wayahudi. Bila shaka! Kwa nini? Alikuwa amelenga; hiyo Dira ya Roho Mtakatifu ilimuweka moja kwa moja katika Nyota ya Kaskazini.

Sasa, kama una kitu fulani kinakuvuta kukutoa kwenye hilo, afadhali ukiache. Hilo ni sawa! Itaelekeza kwenye Neno Lake na ni kwenye Neno Lake tu, kwa sababu Roho Mtakatifu alikuja kudhihirisha au kuonyesha ahadi ya Mungu. Hakuna kanuni ya imani itakayofanya hayo; hakuna dhehebu litafanya hilo; hamna mamlaka, wala cho chote kile kinaweza kufanya hivyo, ni Roho Mtakatifu tu kwa Neno; na Yeye ni Chembechembe ya Uhai.

Sasa, hebu chukua punje ya ngano, punje nzuri ya ngano, lakini haiwezi cho chote—kufanya cho chote; imekufa mpaka chembechembe ya uhai inapoingia kwake, ndipo huzaa punje nyingi za ngano. Na Kristo ndiye Uhai ule, ile Yakini. Kama ngano haina hiyo Yakini ndani yake, kamwe haitainuka. Kama hiyo ngano haina Yakini, labda ni nzuri sana kwa nje, lakini haiwezi kuishi, kwa sababu hakuna kitu ndani yake cha kuishi kwacho. Lakini ipatapo ile Yakini, yaweza kuangalia mbele ya watoa makosa wote na kusema, “Nitainuka tena.” Kwa sababu gani? Kwa sababu ina ile Yakini. Iko ndani yake, haina budi kufufuka tena.

Na wakati hiyo... “Kama mkikaa ndani Yangu, na maneno Yangu yakikaa ndani yenu, basi ombeni mtakalo.” Hiyo ndiyo ile Yakini. Lakini kama mna kanuni za imani na kila kitu vimefunanganisha katika hilo... Huwezi kuchanganya mafuta na maji. Unaweza kuvichukua tu na kuvivinjavunja utakavyo; kamwe havitachanganyikana ni kwa sababu ni kemikali mbili tofauti. Na huwezi kufanya kanuni ya imani na Biblia, kinyume cha Biblia, kuchanganyikana. Huwezi kufanya dhehebu na utawa wa kuzaliwa huru—au wokovu wa kuzaliwa huru vichanganyikane pamoja, sababu bila shaka, Mungu hushughulika tu... Nitalinena kwa vyo vyote.

Mungu kamwe havunji mpango Wake. Hawezi kuuvunja, kwa sababu Yeye hana mwisho. Na natambua, mwajua, mimi—inanenwa mbele ya watu wengi. Unaona? Lakini Mungu hawezi kuvunja mpango Wake. Hawezi kufanya jambo fulani siku moja, na kulibadilisha na kufanya kitu, na kusema amekosea siku hiyo.

Mungu hashughuliki na vikundi vya watu; anashughulika na mtu binafsi, kwa sababu watu wana mawazo tofauti; ameumbwa tofauti katika asili. Na Mungu yambidi achukue mtu yule, na kumtatiza, na kumtoa katika utu wake mwenyewe, mpaka amfanye kuwa na tabia Yake; ndiposa Mungu anamshughulikia mtu huyo.

Angalia kupitia nyakati zote, Nuhu na Musa, manabii wale, hamna wawili kwa wakati ule ule—mmoja, mfululizo kupitia nyakati zote. Kwa hiyo, kama ukisema, “Katika mausia ya watu wengi kuna usalama” . . . Liangalie!

Kama nilivyohubiri hapa kwenye maskani, si muda mrefu uliopita, kulikuwa na Ahabu, na kulikuwa na Yehoshafati. Nao walikuwa wakielekea Ramothi iliyo Giliadi kusukuma. . . Kimsingi walikuwa sahihi, nchi ile ilikuwa yao. Na a—adui, Waashuri kule walikuwa wakishibisha matumbo ya watoto wao kwa ngano ambayo Israeli wangekula—mali waliyopewa na Mungu. Kwa hiyo kimsingi lilionekana kuwa jambo zuri. “Enenda pamoja nami, kwea huko, nasi tutawafukuza watoke nchini.” Vema, hilo lilisikika zuri sana; kimsingi lilikuwa sawa, lakini ni masharti.

Yehoshafati, akiwa mtu mzuri, alisema, “Lakini je, hatupaswi kumuuliza Bwana?”

Bila shaka, Ahabu, huyo aliyerudi nyuma, alisema, “Vema, hakika” (mwamini hadi mpakani, wajua). Kasema, “Lo bila shaka, ningaliwazia hilo. Ninao manabii wa Kiebrania mia nne—mia nne wao ninaowalisha, ninaowatunza. Ndio wazuri sana nchini. Tutawaleta.”

Na wote pamoja kwa moyo mmoja walisema, “Nenda; Bwana yu pamoja nawe.” Kimsingi walikuwa kweli, lakini hawakuwa wameshika ile Yakini.

Basi aliposema, “Hakuna mmoja zaidi?” . . .

Kasema, “Naam, kuna mwingine, bali namchukia.” Akasema, “Yeye hunena maovu dhidi yangu siku zote (mnaona?), kila mara anasema. . . .”

Angeweza je kutabiri mema, huku Neno lote. . . ? Eliya, ambaye alikuwa kabla yake, alimwambia Ahabu, “Mbwa watairamba damu yako.” Sasa, iweje nabii yule aliyedhihirishwa anene kitu cho chote ambacho hakikuwa mapenzi ya Mungu? Na jinsi ambavyo mbwa wangemla Yezebeli, na mavi yatakuwa makondeni, ili hawangesema, “Hapa amelala Yazabeli.” Kukiwa na laana kama hiyo juu ya mtu, mtu mwingine angeweza je kumbariki?

Hivyo ndivyo ilivyo siku ya leo. Mtu anaweza je kubariki mambo haya ambayo yanawachukua watu mbali na Mungu wakati wote? Kuna kitu kimoja tu cha kufanya. Hata kama

itakulazimu kusimama peke yako, kilaani kitu hicho katika Jina la Bwana na ukae nalo, wakati una hakika . . .

Nawe unasema, “Vema, Ndugu Branham, unawafanya watu wakuchukie.”

Mungu atanipenda. Hiyo ni—hiyo ndiyo Yakini yangu. Siwezi kutumainia mkono wa nyama, inakubidi kusimama katika Neno, yale ambayo Mungu alisema utende.

Mikaya alijua alikuwa sahihi? Alingojea, alikuwa na ono. Walikuwa na ono pia, lakini ono lile halikulingana na Maandiko. Na leo ni jambo lile lile. Mikaya alilinganisha ono lake na Neno, kisha aliona yeye na Neno walikuwa pamoja. Leo, kama ono lako ni kinyume cha Neno, liache, sababu ni yakini isiyo sahihi. Yakini ya Mikaya ilipatana na Neno, hivyo aliweza kusimama na kusema, “Yeye. . .”—alilosema na—na kuliadini. Walipompiga kofi la mdomoni na kusema, “Alitokaje kwangu Roho ya Bwana?” alisema, “Utaona siku ile utakapoingia katika chumba cha ndani.” Sawa.

Alisema, “Nitakaporudi kwa amani. . . Mtieni mtu huyu gerezani, kisha nitakaporudi kwa amani,” akasema Ahabu, “Nitapambana na mtu huyu.”

“Lo sasa, Mikaya, vipi basi? Kichwa chako kitakatwa atakaporejea!

Mikaya alisimama hapo kwa ukali kama Stefano alivyofanya (Amina!), bila kusitasita tu kama Bwana wangu alivyokwenda msalabani, kwa urahisi kama Danieli alivyoenda kwenye tundu la simba, au Shadraka, Mishaeli, Abednego walivyokwenda kwenye ile tanuru. Hakika! Alisimama hapo akasema, “Ukirudi kabisa. . .” Kwani? Alikuwa na hakika. “Ukirudi kabisa, Bwana hakusema kwa mimi. Basi ukate kichwa changu.”

Alikuwa na Yakini. Alijua kwamba Dira yake, ambayo imemuongoza kwenye ono hili, ilikuwa inapatana kabisa na Nyota ya Kaskazini. Ndiyo, Bwana! Nanga yake ilishikilia. Ndiyo, Neno na Hilo tu. . .

Kama Yakini yako, kama una Yakini katika maisha yako. . .

Kulikuwa na wakati ambapo, wajua, maadili yalikuwa na yakini. Siwezi kukumbuka jina la mwanamke yule, lakini taifa zima lilitegemea kile alichonena mwanamke yule. (Ninasahau jina lake. Nilikuwa nikiandika mambo machache hapa; singelikumbuka jina la mwanamke yule—ni nani.) Lakini hapa miaka michache iliyopita iliwapasa wawe. . . Mwanamke huyu, lile alilosema. . . Kama alisema utumie kisu katika mkono wa kushoto, ilikuwa—ilikuwa hivyo tu; hilo lilikuwa neno la mwisho. Yeye alikuwa—alikuwa jawabu ya yote. Na kama ulishika uma kwa mkono wa kiume, basi ulikosea kabisa. Jina lake lilikuwa nani? [Kusanyiko linajibu, “Emily Post”—Mh.] Lo, naam, hakika. Ndio, huyo ndiye.

Sasa, mlikuwa—mlikuwa yakini—na yeye alikuwa—alikuwa yakini ya maadili. Lazima iwe namna hiyo. Kama, lo, mambo mengi tunayaona kama hivyo. Lakini tunaona sasa haipo. Kula namna unavyotaka. Ndio, bwana! Sawa! Lakini huyo alikuwa yakini ya maadili. Ilikubidi ufanye hilo namna hiyo.

Kulikuwa na wakati ambapo Adolf Hitler alikuwa yakini ya Ujerumani. Lo lote alilosema . . . Aliposema “Ruka!” waliruka; aliposema, “Uwa!” wanauwa. Mamilioni ya Wayahudi, alitikisa kichwa chake. Unaona kilichotokea kwa yakini ya namna hiyo? Ilionekana kama mamlaka, lakini ilikuwa kinyume cha Neno.

“Wajuaje ilikuwa kinyume cha Neno?”

Mungu alisema . . . Si ilikuwa Baalamu ambaye alijaribu kuwaangalia Israeli kutoka juu apate kuwalaani, alisema, “Ninamuona kama nyati. Mahema yako ni ya haki namna gani. Akulaaniye atalaaniwa; akubarikiye atabarikiwa.”

Yaonekana kama kwamba Hitler angeona hilo. Yaonekana kama kwamba hao Wakristo wa Kijerumani wangeweza kuona hilo. Unaona? Hiyo yakini . . . Kinyume kabisa cha lile Neno . . . Unajua, kama ilivyokwisha kusemwa, “Mwanadamu—Mungu alimuumba mwanadamu, lakini mwanadamu alifanya watumwa”—mmoja akijaribu kumtawala mwingine. Tuna Mtawala mmoja, huyo ni Mungu.

Lakini Hitler alikuwa yakini ya Ujerumani. Angalia hilo leo. Sasa, unaona lililotokea? Ilikuwa yakini baya. Kwa nini? Ilikuwa kinyume cha Neno! Na sasa, unaona yote yalikoishia? Aibu.

Na kama yakini yako ni katika dhehebu fulani au mshutuko fulani, au kitu kingine mbali na Utu wa Yesu Kristo, utafikia kwenye sehemu iyo hiyo ya aibu, ila tu baya zaidi. Unaona? Kama yakini yako si Kristo, huyo ndiye Nguzo ya Kati ya maisha ya mwanadamu; na Kristo ni Neno, si kanisa lako, neno lako, Neno. Unaona? “Juu ya Yakini hii nitalijenga Kanisa Langu”—juu ya Kristo, Neno.

Kulikuwa na wakati ambapo Mussolini alikuwa yakini ya Rumi. Sijui, huenda nilisoma nakala fulani, au ingewezekana kwamba nililisoma katika kitabu, au mtu fulani aliniambia, lakini mtu fulani alipokuwa anahojiwa na Mussolini alikuwa—alikuwa—alitaka kuingiza Rumi katika mwana riadha—riadha. Na kuna sanamu yake kubwa iliyokuwa ikisimama pale kuhusu riadha. Hilo ni kweli! Uyunani ilikuwa na wazo hilo miaka mingi iliyopita. Rumi siku zote ilijaribu kuwa nalo. Riadha ni sawa, lakini—lakini—riadha, lakini—lakini kumbuka, hiyo haitachukua mahali pa Kristo. Haidhuru una nguvu jinsi gani, hilo si kitu. Yeye ndiye nguvu zote.

Na unaona kile alichotaribu kuijengea Rumi juu yake? Na alijaribu kuijenga Rumi juu ya jambo la yakini; kwamba yeye alikuwa ndiye hiyo yakini. Nao walisema kwamba siku moja kwamba motokaa ya—yake—dereva wake alifika dakika moja

mapema, naye akampiga risasi. Akasema, “Sikusema uwepo hapa saa tatu dakika moja, nilisema uwe hapa saa tatu!”—plowy! na kumpiga risasi. Unaona? “Sikutaki hapa dakika moja mapema; nakutaka hapa saa tatu!” Unaona? Angalia ni yakini ya namna gani aliyotaka kujifanya mwenyewe. Lakini unaona kilichotokea?

Mnakumbuka (wengi wenu hapa, watu wa zamani, Roy Slaughter labda, na nyuma zaidi huko) mnakumbuka chini kule nilipowaambia kwa unabii? Siku moja chini kule kwenye jumba la Odd Fellow, kabla hatujawahi kuja hapa, nilisema, “Mussolini ataisha kwa aibu!” Nilisema, “Uvamizi wake wa kwanza, atakwenda Ethiopia; na Ethiopia itaanguka miguuni pake, lakini itafikia mwisho wake, na hakuna atakayemsaidia; na atazikwa kwa aibu.” Yupo hapo.

Nilisema, “Kuna imani tatu za siasa zilizoinuka, unazi, ufashisti na ukomunisti.” Nilisema, “Hizo imani za siasa zitazunguka na kuishia katika moja; itakuwa ukomunisti. Angalia! Ukomunisti utaiteketeza Rumi.” Mnaona? Wewe uangalie. Ni chombo katika mikono ya Mungu. Wanafikiri wanampinga Mungu, na wanatenda moja kwa moja kutimiza hilo wakati wote, hawajui. Anawatumia tu kama kibaraka, chombo fulani mkononi Mwake, kama alivyofanya na Nebukadreza na wengi wa hao wengine.

Sasa tazama! Unaona? Sasa, kulikuwa na wakati Farao alipokuwa yakini ya Misri, lakini angalia sasa ilipo. Unaona? Yote hushindwa. Lo, ni ya aina baya, kwa hiyo siku zote hushindwa. Hizo ni yakini zilizofanywa na wanadamu. Hamwezi kutwaa yakini iliyofanywa na mwanadamu, sijali kama ni ra—rais, kama ni mtawala wa mabavu, kama ni Mfalme, kama ni kanisa, kama ni dhehebu, kama ni kanuni ya imani, cho chote cha vitu hivyo vitaangamia, kama yakini zote za aina hiyo katika nyakati zote.

Twaweza kuangalia nyuma... Angalia nyuma! Angalia watu waliotumainia watawala wa madola; angalia watu waliotumainia watawala wa mabavu; angalia watu waliojenga matumaini yao katika yakini za namna hiyo; na angalia walipo leo!

Sasa, hebu tugeuke na tutazame watu ambao waliweka matumaini yao juu ya Biblia, juu ya Neno la Mungu na wakalishikilia kama Yakini; angalia walipo sasa.

Paulo anakupa maelezo mafupi ya wao katika Waebrania sura ya 11: walivyofanya, jinsi ambavyo walishinda falme, wakatenda haki na kadhalika, nao walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao, wakingojea utukufuni ule Ufufuo wenye fahari sana. Unaona? Sawa! Kwani wao... Baadhi yao ha—hawakupata miujiza hii, nao waliitoa miili yao kwa

vyo vyote, wakiutazamia Ufufuo ule. Kumaliza maisha yao, hawakuyajali, walitaka kuendelea kujitoa kafara, ili waweze kupata Ufufuo ule; na hilo ndilo walilotenda.

Sasa, yakini... Tunazungumzia... Yakini... Unajua, Mahakama yetu Kuu ni yakini. Ni yakini; ni—ni mwisho wa mabishano yote katika taifa hili. Hilo ni sawa. Uamuzi wao ndio yakini; katika Mahakama yetu Kuu. Hilo ni kweli. Lo, najua wakati mwingine hatulipendi hilo, lakini ni—ni yakini kwa vyo vyote vile. Ndio bwana. Vipi kama hatukuwa nayo, nini basi? Lakini hayo ndiyo yakini. Ndivyo hasa. Kwa nini? Hilo ni—taifa letu limefunGANishwa nayo.

Wakati Mahakama hiyo Kuu mwishowe inafanya uamuzi wake wa mwisho, basi, hakuna... Utakwenda wapi baada ya huo? Utakwenda kufuata uamuzi wao, hayo tu; inakubidi kufanya hivyo. Wao ndio neno la mwisho; wao ni “Amina.”

Waweza kufanya kesi katika mahakama ya hapo mjini; unaweza ukaipeleka kwa jaji mdogo, na kisha uende kwa mkoa—kwa mahakama za aina yo yote, na kwa mahakama ya mkoa, lakini tunapokuja kwenye Mahakama Kuu, basi. Hiyo ni kweli. Wakati mwingine hatutaki ku—kusema, “Vema, sitaki uamuzi wao,” lakini jaribu kuupuuza wakati mmoja. Hiyo ndio yakini ya taifa. Vipi basi kama hatukuwa nayo? Ndio.

Inatubidi tuwe na yakini. Kila mtu yambidi awe na moja. Una moja. Lakini ninayotaribu kuwaambia, kujenga msingi hapo na kuwaonyesha yakini ni nini.

Sasa, Mahakama Kuu ya taifa ndiyo yakini ya taifa. Hicho ndicho kitu cha mwisho katika ugomvi wa namna yo yote. Hulisawazisha. Wasemalo, ndilo hilo.

Kuna yakini kwenye mchezo wa mpira. Huyu ni refarii. Lo, ndio! Wakati mwingine hatutaki uamuzi wake hata hivyo, lakini ni—ni—ndio huo kwa vyo vyote. Refarii, uamuzi wake ndio neno la mwisho. Hiyo ni kweli. Haidhuru wengine watasemaje; kama akisema ni goli, ni goli. Hiyo ni kweli! Bila shaka. Haidhuru wengine watasemaje, hayo hayahusiani na hilo. Hebuni tufikirie... Kama wewe ni... (Siendi kwenye michezo ya mpira, lakini hata hivyo niliandika hilo.) re—refarii, ndiye yakini kwenye mchezo wa mpira.

Mmoja wao aseme, “Goli limeingia!”

Mwingine aseme, “Wewe ni mwongo!”

Huyu aseme, “Hili si *hivyo*; inambidi awe namna *hii*.”

Refarii alisema, “Goli!”

Unaona? Wengine wao wanachukua viti vyao na kuketi. Wanagombana, baadhi yao, lakini... Nafikiria wangemzomea mioyoni mwao na kadhalika, lakini ni goli hata hivyo. Kwa nini? Yeye ndiye neno la mwisho.

Mchezaji wa kwanza anasema, “Unajua huo, huo ulipita!”

Mwingine asema, “Wajua hilo si sawa!”

Angesema, “Goli!” Hayo tu. “Fungeni midomo yenu basi, rudini mahali penu.”

Vipi kama kusingekuwepo refarii kwenye mchezo wa mpira? Jamani, ungewazia ungekuwa mchezo wa namna gani? Mmoja wao alisema, “Lilikuwa goli!”

Mwingine alisema *hili*.

Mwingine alisema *lile*.

Mwingine alisema, “Mwongo we!”

Wangukuwa wanagombana na kupigana. Kucheza mchezo wa mpira, inakubidi uwe na yakini. Naye hutembea nje kule, na haidhuru kama humpendi au nini, yeye—yeye ndiye neno la mwisho kwa vyo vyote. Yeye ndiye yakini hata hivyo. Ndiye yakini; ndiye neno la mwisho. Haidhuru utasemaje kuhusu hilo, ndivyo ilivyo. Sasa, kama hawangetenda hayo, mchezo wote ungeingia katika machafuko. Sivyo?

Taifa lingekuwa kama kusingelikuwa na mahakama ya taifa? Kama kusingekuwa na Mahakama Kuu katika taifa hili, je, lingeelekea wapi—lingeelekea wapi? Taifa lingekuwa katika machafuko.

Kama kusingekuwa na—kama kusingekuweko na refarii kwenye mchezo wa mpira, ungeishia—usingeutupa mpira wa kwanza, kabla ya mtu kuleta ugomvi. Mtu fulani asimame pale na pengine ile—kweli ilirudi upande wake, na mtu yule mwingine angesema, “Lo, la! La, la la! Haikufanya hivyo!” na kisha hali inakuwa hivyo. Mpira wa kwanza utupwe, wataubishaniana. Mmoja wao alisema, “Hilo lilikuwa goli!”

Wangesema, “Halikuwa goli!”

Unaona? Yakubidi uwe na mtu ambaye mchezo umefungwa kwake, na huyo ni refarii. Wakati anaposema, “Goli!” ni goli. Kama akisema, “Mpira!” ni mpira. Kila asemacho, kinakubaliwa. Ndivyo mambo yalivyo! Na kama hamumkubalii, hamwezi kucheza mchezo.

Hebu niwaonyeshe yakini nyingine. Kuna taa nyekundu, taa nyekundu. Wakati isemapo, “Simama!” inamaanisha simama! Kama ukiendelea, utajuta. Lakini kama mji huu haukuwa na taa zo zote hapa, taa za trafiki za kusimamisha, ungekuwa mji wa namna gani? Hapana budi kuwe na yakini. Sijali polisi alisema nini au mtu mwingine ye yote anayesimama pale; wao si muhimu.

Kama mtu fulani anaweza kuthibitisha ya kwamba ulipita wakati wa taa za kijani, sijali polisi alisema nini, wamekosea. Taa aliposema, “Nenda!” hilo lilimaanisha nenda. Hiyo ndiyo yakini. Unaweza kuthibitisha hilo, taa ilisema, “Nenda!”

Huenda ikawa polisi alikuwa amesimama mahali fulani, labda meya wa mji, mahali fulani, hilo halijalishi hata kidogo. Kama una thibitisho kwamba ilikuwa “nenda,” wewe nenda; na kama mtu fulani akikugonga, ni kosa lao. Waweza kuthibitisha. Hiyo ni kweli. Twaweza kuthibitisha kile tunachozungumzia. Hiyo ni kweli.

Sasa, vipi kama kusingekuwepo na taa nyekundu? Mtu afikapo kwenye njia panda, ina- . . . Tazama jinsi kungekuwa. Mmoja asema, “Wewe, simile; nina haraka. Sina budi kwenda kazini; nimechelewa sasa. Napita sasa.”

Mwingine asema, “Unajifikiria tu eti unapita, kwa sababu mimi ndiye nitakayepita, kwa sababu nilikuwa wa kwanza hapa.” Na naweza kuona mwanamke akitoka na kutengeneza nywele zake.

Vipi kama tusingekuwepo na taa nyekundu? Si kungekuwepo na msongamano wa magari!

Hivyo ndivyo ilivyo kwa makanisa. Unaona? Hilo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu tuna msongamano mkubwa hivyo wa kidhehebu. Hilo ni sawa kabisa. Hakuna anayepiga hatua, wamesimama, wakigombana.

Nuru ya Mungu iko hapa. Isemapo, “Nenda!” nenda. Isemapo, “Simama! Umekwenda vya kutosha!” basi simama. Hiyo ni kweli. Hapa ndipo tulipoweka msingi wetu, hilo, hilo Neno, si yale baadhi ya kundi la watu lilisema au kundi la watu wengine lilivyosema.

Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Hebu twendeni! “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.”

Unajua, ingawa elimu ni nzuri, lakini Yesu kamwe hakuamrisha hiyo. Hiyo ni kweli. Ingawa makanisa ni mazuri, majengo, kamwe hakuamrisha hayo. Hospitali ingawa ni nzuri . . . Sisi—makanisa hujenga mahospitali. Hilo ni sawa, tunathamini hilo, lakini Yeye hakuamrisha hayo.

Aliliambia kanisa, “Hubirini Injili.” Na Injili hiyo haikuja kwa Neno tu, lakini kwa nguvu na udhihirisho wa lile Neno. Paulo alisema hivyo. Basi enendeni mkadhihirishe Injili. Lo, jamani! Kama ilikuwa hivyo . . .

Lo, leo twaishi katika wakati ambapo tunao madaktari wazuri sana kuliko tuliowahi kuwa nao. Tuna dawa nzuri sana tulizowahi kutumia. Mwajua hilo. Nasi twawaheshimu watu hao, tunawaomba. Mimi ninawaomba, na natumaini mnawaomba. Watu hao ambao pamoja na kuelewa kwao kwa kujihisi. . . Wanazo hisi mbili wanazotumia, ambazo ni kuona, na kuhisi, na wao—na kusikia. Wanafanya kazi kwa mpigo wa moyo, au ku—kuhisi uvimbe au kitu fulani, au kuona kitu fulani wanachoweza kuona, kuenea kwa ugonjwa, au—au kitu fulani

usoni ambacho kinafunika uso au mwili mahali fulani. Wao—wao wanatenda kazi wakitumia mambo hayo (unaona?), kwa sababu hilo ni... Hujaribu kunywa madawa, na kiasi fulani ambacho kitayauwa, wala hayakuuwi, na na—na kadhalika. Hawata... Hiyo ni kazi yao kushugulikia hilo. Nasi twalipenda hilo; hilo ni sawa kabisa.

Lakini, tunao madaktari wazuri sana, madawa mazuri sana, hospitali; na maradhi mengi kuliko tuliyowahi kupata. Tuna kutokuamini kwingi kuliko tulikowahi kuwa nako. Ndiyo, bwana! Hilo ni kweli kabisa.

Wahudumu wamejifanyia taratibu, na wakapata madhehebu makubwa, na kuingiza cho chote, na kadhalika (na kwa cho chote wakifanyiza washiriki wa kanisa); na wamechukuliwa na seminari, kama kuku aliyeatimiwa kwa mtambo (na kuanguliwa kwa—kwa kisaga cha kusagia ambacho huwatoa hivyo), na wakati mwingine hawajui zaidi kumhusu Mungu kuliko Mhotentoti anavyojua kuhusu hekaya za Kimisri. Kuwaleta kuwapitisha hivyo, na yule... Ndivyo hivyo. Unaona?

Lo, tunalohitaji katika makanisa yetu ni mtu aliye na Yakini! Tunalohitaji katika kanisa la Kimethodisti, kanisa la Kibatisti, kanisa la Kipentekoste, kanisa la Kipresbeteri ni Yakini—mtu wa Mungu ambaye atasimama amefungiwa kwenye Neno na kwa Kristo, na kulileta kusanyiko hilo chini ya hali ambapo kila mwamini huenenda katika masharti ya Neno hili, akiona Neno hilo limedhihirishwa, likifuata, “Ishara hizi zitafuatana na hao kuamini, katika ulimwengu wote.”

Walisema, “Hilo liliisha.”

Yesu alisema “Enendeni ulimwenguni mwote, hubirini Injili kwa kila kiumbe.”

Bado hatujaufikia ulimwengu wote, na tuko mbali sana na kila kiumbe. Umbali gani? Ulimwenguni mwote. Kwa akina nani? Kila kiumbe. Itakuwaje? “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kwa Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya; kama watashika nyoka au kunywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

Hiyo ndiyo Yakini ikishikilia pale, lile Neno, Nyota ya Kaskazini, dira ambayo hukaa nayo. Hicho ndicho tunachohitaji.

Lakini tumetoka na kujenga taasisi, kuwaunganisha watu, kuingiza washiriki, na kugombana na Wabatisti (kwa sababu hawakuamini jinsi tulivyoamini) na Wamethodisti kwa sababu hawakufanya namna hii); nasi tukaangua seminari kubwa zaidi, na kujenga makanisa makubwa zaidi, viti vizuri zaidi, na kinanda kikubwa, na kadhalika, na kundi kubwa lililovalia vizuri zaidi; wanaye meya na kila mtu kanisani; nasi tuna

nini? Kundi la maiti, lililofungiwa kwenye yakini ya kidhehebu! Mauti! Lo, hashu!

Kama nikifa katika safari yangu, Yakini yangu ni Yesu Kristo; naamini Hilo. Kama kila mtu akitoka nje... Mtu fulani alisema—Dakta Davis aliniambia, “Billy, ukihubiri kitu kama hicho, utakihubiria nguzo za kanisa.”

Nikasema, “Nitakuwa nikihubiria hizo nguzo Neno la Mungu basi, sababu Mungu aweza katika nguzo hizi kumwinulia watoto Ibrahimu.” Sawa! Neno la Mungu ni kweli!

Kasema, “Unafikiri watakuamini?”

Nikasema, “Hilo si shauri langu. Jukumu langu ni kudumu kweli na Neno hilo.” Hilo ni Kweli.

Nikasema, “Si Uponyaji wangu wa Kiungu, ni ahadi Yake. Yeye ndiye aliyetoa lile agizo.”

Lo, nami nakumbuka aliposhuka chini pale katika Nuru ile kuu, nikisimama kule kwenye kina cha mto, 1933, mnamo Juni, aliposema, “Kama—kama Yohana Mbatizaji alivyopelekwa na kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, nakupeleka wewe na Ujumbe kwa walimwengu kutangulia kuja mara ya pili kwa Kristo.” Nao umezunguka ulimwengu ambapo mioto ya ufufuo iliisha washwa kwa miaka kumi na mitano katika karibu kila mlima. Uponyaji wa Kiungu katika mataifa yote, na nguvu, na kurejeshwa, na sasa, naamini uko tayari kugonga kilele kile cha mwisho kule kuleta imani ambayo italinyakua Kanisa hata Utukufuni; na lipo katika hizo Jumbe! Kweli tuko katika wakati wa mwisho. Tumekwisha kulizungumza na kila kitu, lakini jambo hilo limetufikia sasa. Wasikilizeni! Naam, bwana! Hapa yupo mmoja! Hiyo ni kweli!

Taa nyekundu, kama nilivyosema, huamua mambo! Hivyo tu. Taa nyekundu inakuambia nani apitaye. Haidhuru mtu ye yote asema nini, ni lile ambalo taa nyekundu isemalo. Unaweza kwa kweli kuwa na msongamano wa magari usipofanya hivyo; kama hujali hiyo taa nyekundu. Sharti kuwe na yakini. Naam, bwana!

Kama ilivyo kwa Kanisa, lazima kuwe na Yakini. Kwa watu Kanisani, hamna budi kuwa na yakini yenu. Lakini leo kila kanisa lina yakini yake lenyewe. Unaona? Hawajaribu kuchukua...

“Sisi Wabaptisti huamini *hili*!”

“Sisi Wamethodisti huamini *hili*!”

“Sisi Wapresbeteri huamini *hili*!”

“Sisi Wapentekoste huamini *hili*!”

Hilo ni sawa, lakini kwa nini msichukue hilo lilolobakia? Hilo lililobakia lina nini?

“Sisi Wabatisti tunaamini katika kuzamisha.”

Hilo ni zuri; na basi ubatizo wa Roho Mtakatifu je? Na kunena kwa lugha je? Na karama za uponyaji? Na unabii je?

“Lo, hapana! Hatufanyi hivyo; huo—huo ulikuwa kwa wakati mwingine.” Lo, jamani!

Wapentekoste, mnasema, “Vema, tunaamini katika kunena kwa lugha kama uthibitisho.”

Hakika, kunena kwa lugha ni sawa, lakini, huo bado si uthibitisho. Watu wengi hunena kwa lugha (hilo ni kweli), na hicho ndicho kiwango wanachofikia tu. Ibilisi anaweza kuigiza kipawa cho chote alichacho, kipawa cho chote katika Biblia.

Paulo alisema, “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na malaika; nikijitoa mwili wangu uungue kama kafara; nijapotoa mali zangu zote kuwalisha maskini, na nijapokuwa na imani kiasi cha kuweza kuhamisha milima; nijapokuwa nilienda kwa seminari na kujifunza ujuzi wote uliopo kujifunza, bado si kitu mimi.”

Ni Utu wa Kristo. Kristo! Mpokeeni; na huwezi kumpokea bila ya kulipokea Neno Lake. Yapasa Neno lije kwanza; ndipo uhai utakuja katika Neno lile na kudhihirisha Neno lile.

Je, Yesu hakusema, “Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi”? Ilikuwa Neno la Mungu likidhihirishwa. Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha, akijionyesha Mwenyewe kwa ulimwengu, kile alichokuwa. Hiyo ilikuwa—hiyo ilikuwa Yakini. Hiyo ilikuwa Yakini ya Milele hapo.

Kisha wasema, “Hilo ni la Milele, Ndugu Branham?” Hiyo ilikuwa! “Basi na siku hizi je?”

Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya”—Yakini ile ile. Sawa!

Kila mmoja ana yakini yake. Lo, jamani! Ni kama tu ilivyokuwa katika siku za Waamuzi: kila mtu alifanya lililokuwa sahihi machoni pake mwenyewe. Katika siku za Waamuzi kila mtu alikuwa na yakini—yakini yake. Alitenda tu alilotaka kutenda, na hivyo ndivyo ilivyo sasa. Kila mtu alitenda iliyo sahihi mbele ya macho yake.

Sasa, wajua sababu walifanya hilo katika Waamuzi? Hili linaweza likushtue kidogo. Lakini sababu ya kufanya hivyo katika Waamuzi, ni kwa sababu hawakuwa na nabii katika siku hizo kwa Neno la Mungu kuwajia, kwa hiyo kila mtu angetenda alilotaka machoni pake.

Na hilo ndilo hasa limetendeka siku hizi. Hatuna nabii katika siku hizi za madhehebu, lakini Mungu alituahidia mmoja. Unaona, unaona. Ametuahidi. Katika siku za mwisho atainua na kumpeleka Eliya uwanjani tena, naye ataigeuza mioyo ya watoto kuelekea imani ya baba zao—kurudia Pentekoste ya asili. Wajua alisema hivyo!

Nami najua utarejea, kama alivyomtendea Yohana kule (kule katika—na Mathayo sura ya 11 na mstari wa 6, naamini ni huo) waliposema, “Mnafikiri mtu huyu alikuwa ni nani, huyo Yohana?”

Alisema, “Kama mkitaka kukubali, huyu ndiye aliyeandikiwa haya, ‘Tazama namtuma Mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.’ Hiyo ni Malaki 3, siyo Malaki 4. Lakini kumbuka, kama hiyo ilikuwa Malaki 4, basi Neno halikutimia, kwa sababu yeye alisema lakini mnamo wakati huu ulimwengu wote ungechomwa moto, na wenye haki wangetembea juu ya majivu ya walio waovu. La! Msilichanganye, ndugu zanguni; lifanyeni linene sawa sawa na linavyosema. Hiyo ni kweli. Ameliyahidi katika siku za mwisho, na itakuwa katikati kabisa.

Kumbuka, wakati wa Waamuzi, kila mtu alitenda namna alivyotaka. Hapakuwa na mtu, hakukuwa na mtu angalilifanya hilo Neno kuishi. Hapakuwa na nabii. Neno la Mungu siku zote huja kwa nabii (hilo ni sawa), naye siku zote huchukiwa. Kundi dogo tu ndilo limpendalo! Na . . . Unaona? Lakini ninamaanisha, siku zote hilo limekuwepo.

Mungu habadilishi taratibu Yake; hawezi na awe Mungu. Kama Mungu akisema kitu au akitenda kitu, lazima afanye wakati mwingine. Matatizo hayo yajapo, kama Yeye hatendi mara ya pili jinsi alivyofanya mara ya kwanza, alikosea mara ya kwanza. Na ni nani atamshitaki Mungu kwamba ametenda makosa? Wewe ni nani uweke dhambi juu ya Mungu? Hilo ndilo Yesu alilosema: “Ni yupi miongoni mwenu anayeweza kunishuhudia kuwa nina dhambi?”

Dhambi ni nini? Kutokuamini. “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa tayari.”

“Ni yupi miongoni mwenu anayeweza kunionyesha kwamba sijatimiza kila kitu ambacho angetenda Masihi?” Unaona? Hakuna aliyesema neno. Alitimiza; Masihi alikuwa Nabii, naye aliishathibitisha kwamba alikuwa hivyo. Hawakuwa na nabii kwa mamia ya miaka, tangu Malaki, na hapa anajitokeza. Alikuwa mtu asiyeleezeka kwa watu na jiwe la kujikwaa kwa kanisa lao, sababu Yeye alisema, “Tazama, naweka jiwe katika Sayuni, Jiwe la Pembeni, lenye thamani, lililolaribiwa, lo, jiwe la kujikwaa. (Ndio!) Bali ye yote amwaminiye hatatahayarika.” Hilo ni kweli. Alikuwa pale. Na wao . . . Alitimiza Maandiko sawa kabisa. Lakini wale waliomwamini Yeye walikuwa na Yakini.

Maskini Martha, alipomuona Lazaro akitoka kaburini, alijua Huyu alikuwa nani. Hata kabla ya kulifanya hilo, alikuwa na yakini ya kujua, “Naamini kwamba Wewe ndiwe Mwana wa Mungu yule ajaye ulimwenguni. Hata sasa, ijapokuwa ndugu yangu amekufa, nena neno tu; Mungu atalitenda.” Amina! Alikuwa na uhakika kabisa. Hilo ni kweli.

Aliposema hayo (na yeye alimaanisha hilo toka moyoni mwake), Yeye akasema, “Mmemzika wapi?”

Akasema, “Njoo utazame.”

Hapo alisimama hapo na ono, sababu Yeye alisema, “Sifanyi kitu mpaka Baba amenionyesha kwanza.” (Yohana Mt. 5:19).

Alimpeleka toka—aliondoka nyumbani kwa Lazaro. Walitumana Yeye aje akaombe. Yeye alijua Lazaro atakufa; na baada ya muda fulani, Yeye akasema, “Rafiki yetu, Lazaro, amelala.”

Wakasema, “Anafanya vema!”

Akasema, “Amekufa; na kwa ajili yenu ninafurahi kwamba sikuwako huko.” (Wangemuomba amuombe). Ndipo yuarudi, akasema, “Lakini ninakwenda ili nimwamshe.” Lo, jamani! Siyo “Nitakwenda nione ninaloweza kufanya,” “Nitakwenda kumwamsha.” Kwa nini? “Baba tayari amekwisha nionyesha Mimi la kufanya.”

Akaenda kaburini. Hapo alisimama Mtu; hapo alisimama Mungu katika mwili, ambaye angeweza kuliambia jiwe, “Yeyuka!” na lingeyeyuka; lakini aliwaambia wale akina mama, hao maskini akina mama, maskini akina mama vijana, akasema, “Liondoeni jiwe!”

Una jambo la kufanya pia. Unaona? Nao wakaliondoa lile jiwe; nalo liliwachafua moyo, alikuwa ananuka sana. Hapo alisimama hapo. Lo, jamani! Naweza kumuona akiunyosha maskini mwili huo mnyonge (kwa sababu Biblia ilisema hakukuwa na uzuri tungemtamania; hakuwa kitu cha kuvutia macho. Unaona?)

Kama Daudi tu. Alichaguliwa kama mfalme alipokuwa kijana mdogo mwekundu. Unaona? Wale jamaa wakubwa walisema, “Si ataonekana mzuri akiwa na taji kichwani mwake?”

“Mchukue huyu mwana aliye na umri mkubwa zaidi,” Yese alisema.

Samuel akasema, “Mungu amemkataa.” Akawaleta wanawe wote.

Akasema, “Hamna mwingine?”

“Tunaye mmoja, lakini hataonekana kama mfalme. Naam, ni kijitu kidogo, mabega yameinama, mtu anayeonekana mwekundu.”

“Nendeni mkamlete!” Na mara tu alipokuja akitembea mbele ya nabii yule, Roho alimwangukia. Akakimbia na mafuta yale naye akamumwagia kichwani mwake, akasema, “Huyu ndiye mfalme wenu.” Sawa! Naam, bwana!

Na Yesu alisimama pale huku mabega yakiwa yameinama, labda akianza kuota mvi na huku hajapata bado umri wa miaka thelathini. (Biblia ilisema angeonekana kana kwamba ana miaka

arobaini.) Wayahudi walisema, “Wewe hujafikia zaidi—zaidi ya miaka hamsini, nawe wasema umemuona Ibrahimu?”

Alisema “Yeye Ibrahimu asijakuwako, Mimi niko.” Jamani, lo, jamani! Yohana Mt. 6.

Ndipo twaona, hapa amesimama karibu na kaburi. Alijua ono lile lilikuwa limjie, alijua lazima litukie. “Liondoeni jiwe!” Alikuwa ananuka, amefungwa sanda, alikuwa amekufa kwa siku nne, pua lake tayari limekwisha dondoka, katika muda huo.

Hapo alisimama hapo; akaunyosha mwili Wake mdogo, “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima! Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, lakini ataishi.” Niambie mtu ambaye angetoa tamshi kama hilo! “Yeye aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe! Unaamini hili?”

Akasema, “Ndio Bwana!” Ingawa hakumsaidia, inavyoonekana, alipotumana aitwe, hakuenda, aliita tena; hakwenda. Lakini hapa asema, “Najua Wewe ndiwe Kristo yule ajaye ulimwenguni.”

Akasema, “Lazaro, njoo huku!” Kisha mtu ambaye alikuwa amekufa siku nne... Kwa nini? Nini? Kristo alikuwa na ile Yakini. Alikuwa ameona ono; halingeshindwa. Hilo ni kweli. Halingeshindwa! Yeye alikuwa na uhakika kabisa.

Kisha Martha alikuwa na uhakika kabisa! Kama angeweza kumfanya Yeye atambue kile alichuamini Yeye kuwa, angepokea alichoomba! Sawa! Ndio hao hapo; ile Yakini ilifungana na Neno; na hilo tu.

Kila mtu leo anafanya lile aonalo machoni pake kuwa zuri, kwa sababu hakuna nabii.

Angalia katika siku za Waamuzi. Angalia hilo! Katika siku ambapo (naamini ilikuwa Eliya au Elisha, mmoja wao. Naam!) yule mtoto mchanga aliyekufa... Yule—yule mwanamke Mshunami, alitengeneza...

Eliya alikuwa mtu wa Mungu wa wakati ule, si tu mwalimu mwenye akili nyingi. Kwani, alikuwa mzee aliyetembeatembea. Alikuwa... Angalikuja—angalikuja mlangoni mwako leo labda ungemfukuza. Taifa nzima lilimchukia. Yazebeli na wengine wote walimchukia, kwa sababu yeye—mwanamke aliketika katika Ikulu na kuwafanya wanawake wote watende alivyotenda; na wote walijifananisha naye; na—na Ahabu aligeuzwa—kichwa chake kiligeuzwa kwa uweza wa mwanamke. Hatuko mbali sasa na huo, leo, ni karibu sawa; na ndivyo—ndivyo hivyo. Walikuwa wote wajipendekezao kwa watu na kila kitu—wote walikuwa wamegandamizwa.

Lakini yule kizee mwanamke Mshunami (si mwanamke Mshunami lakini maskini—naam, naamini alikuwa Mshunami), alipokuja na kuona kwamba uwezo ule ulikuwa katika Eliya, alisema, “Natambua kwamba yeye ni mtu mtakatifu.” Na wakati

yule mtoto mchanga alipokufa, yeye alisema, “Mpande nyumbu yule na usisimame!” Akapanda akaenda kule... Alijua... Nami napenda hilo, jinsi alivyokuja; alifikia kwenye yakini yake, nguzo yake ya kujishikilia.

Eliya alisema, “Hapa yuaja yule mwanamke Mshunami. Ana huzuni, lakini sijui kuna tatizo gani.” Unaona, Mungu haonyeshi watumishi Wake kila kitu, ni lile tu ambalo anawataka wajue.) Kwa hivyo alisema, “Moyo wake una huzuni, lakini sifahamu.” Alisema, “Kimbia, ukachunguze, Gehazi, uone kuna matatizo gani.”

Alisema, “Hujambo? Mume wako hajambo? Mwanao hajambo?”

Mwangalie. Lo, jamani! Naam. Alisema, “Hawajambo.” Kwa nini? Amefikia yakini yake. “Hawajambo.” Naye akapiga magoti... Kwanza alianguka miguuni pake, na Gehazi akamwinua. Hilo si sahihi mbele ya—ya bwana wake, akamwinua; naye akaanza kusimulia.

Sasa, hakuwa na yakini sasa. Alijua alikuwa na nguvu za lile ono kumpa yeye mtoto, lakini sasa, angefanyaje? Alichukua fimbo yake akashuka kwenda chumbani mle, akaweka—akafunga milango yote, akamtoa kila mtu nje. Akatembea huku na huko mle chumbani. Alikuwa na Yakini kama tu angaliweza kuigusa. Mbele nyuma, huku na huko chumbani. Lo, jamani! Moja kwa moja alihisi kitu kinamgusa; akajilaza juu ya kile kitoto kichanga, akainuka tena, akaenda zake. Yule—yule mtoto mchanga kwa namna fulani alianza kusogea, akapata joto. Akainuka mbele nyuma; hakupata kugusana vizuri na Yakini ile. “Ilikuwa nini Bwana? Wasema nifanye nini?”

Bila shaka alipogeuka, aliona ono: yule mvulana mdogo akikimbia, akiruka katika kamba, kitu kama hicho—akicheza. Akajitupa juu ya yule mtoto; akalala pua kwa pua, mdomo kwa mdomo; na Nguvu za Mungu zikamwinua yule mtoto akawa hai. Ilikuwa nini? Yakini ya yule mwanamke ilikuwa nabii, Yakini ya yule nabii ilikuwa Mungu. Na pamoja na Neno, “Mimi ndimi Ufufuo na Uzima, nguvu za Mungu, huyo Muumba.”...? Akafufuka tena, yule mtoto.

Hakika! Sababu ya kila mtu kuenenda katika njia yake ni kwa sababu hawakuwa na nabii ambaye Neno la Bwana lingemjia. Neno na manabii vilikuwa vinakosekana katika siku ile.

Lo, nimeona hili kwenye wongofu wangu, juu ya siku ile tulimoishi. Ninafurahi sana kwamba Mungu alinishika kabla kanisa halijanishika. Labda ningekuwa kafiri (naam, bwana!), mimi—msongamano wote huu wa machafuko na kila mtu. “Vema, njoo ukajiunge na letu. Na kama hujiungi, vema, waweza kuchukua barua yako uende ukajiunge na jingine.” Lo!

“Si ulete barua yako katika ushirika wetu?”

Naamini kuna barua moja; hiyo ni wakati Kristo anapoliandika jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Humo ndimo tu ambamo jina lako limo.

Nilipoona madhehebu yote . . . Asili yetu ni Waairishi, ambao kwanza walikuwa Wakatoliki, nami niliona kwamba hiyo ilikuwa chafu na imeoza. Nilishuka nikaenda kanisa fulani la kidhehebu mjini hapa; walisema, “Lo, sisi ndio njia, kweli, nuru; tuna kila kitu.”

Nilikwenda kwa nyingine huko New Albany. “Lo, jamani! Hao jamaa huko hawajui wanachonena.”

Wakatoliki walisema, “Nyote mmekosea.”

Nikafikiri, “Lo, jamani!”

Nilicheza na mvulana mdogo wa Kiluteri, nami nikafikiri—Mjerumani mdogo wa Kiluteri; nilikwenda huko na nikasema, “Unahudhuria kanisa gani?”

“Naenda kwenye kanisa *lile*.”

Nikashuka nikaenda, nikaona walisema wao walikuwa ndio njia. Kisha nikashuka nikaenda kwa Ndugu Dale, katika Batisti ya Immanueli, au Batisti ya Kwanza; walisema “*Hii* ndiyo njia.”

Kisha nilikwenda kwa kanisa la Kiairishi, walisema “Lakini *hii* ndiyo njia.”

“Lo, jamani! Nimechanganyikiwa sana; sijui la kufanya. Lakini nataka kuwa sahihi!” Sikujua la kufanya, na sikujua jinsi ya kutubu. Niliandika barua. Nilifikiri, “Nimemuona msituni.” Nikamwandikia barua; nikasema:

Kwa Bwana Mpenzi,

Najua Wewe hupita njia hii hapa, sababu nimekaa hapa nikiwinda kindi. Najua Wewe hupita hapa, na najua upo hapa. Nakuhitaji. . . Nataka kukuambia jambo fulani. . .

Nikawazia, “Sasa, ngoja kidogo. Si—sijawahi kuona mtu ye yote siku. . . Nataka kuzungumza nao; na—nataka kuzungumza nao. Na—nataka kuzungumza na Yeye.” Nikafikiri, “Vema sasa, sijui namna ya kulitenda.”

Na nilikwenda nje kwenye kibanda nikapiga magoti, maji, nimelowa na motokaa ndogo imesimama pale imeharibika. Na nikasema, “Naamini nimeona picha. . . Naamini wanaweka mikono yao *hivi*,” nami nikapiga magoti. Kisha nikasema, “Sasa, nitasemaje?” Nilisema, “Kuna njia fulani ikupasayo kufanya hivi, nami sijui. Najua kuna njia ya kuendea kila kitu, na mimi si. . .”

Nilisema (niliweka mikono yangu *hivi*)—Nikasema, “Bwana Mpenzi, ningependa kwamba ungekuja na kuzungumza nami kwa muda kidogo. Nataka kukuambia jinsi nilivyo mbaya.” (Nilishikilia mkono wangu *hivi*.) Nikasikiliza. Watu

walisema. . . Mungu alizungumza nami, na nalijua alizungumza, sababu nilimsikia nilipokuwa mtoto mdogo, akiniambia nisinywe pombe na kadhalika. Hakunijibu.

Nikasema, “Labda nilipaswa kuweka mikono yangu *hivi*.” Kwa hivyo nilisema, “Bwana mpenzi, mimi—mimi sijui namna hasa ya kufanya hili, lakini na—natumaini ya kwamba uta. . . Utanisaidia?”

Na kila mhubiri akiniambia niende nikajiunge na lao, na kusimama na kusema wamempokea Yesu Kristo, na wanamwamini Yesu kuwa Mwana wa Mungu. Mashetani wanaamini jambo lile lile, kwa hiyo nikafikiri, “Ya—yanipasa kuwa na kitu bora zaidi ya hicho.” Kwa hivyo nilikuwa nimeketi *hivi*.

Nilisoma ambapo Petro na Yohana walipitia mlango uitwao Mzuri, na palikuwa na mtu aliyekuwa kiwete tangu tumboni mwa mama yake. Kasema, “Mimi sina fedha wala dhahabu, lakini nilicho nacho. . .” Nalijua sikuwa na hicho.

Kwa hiyo nilikuwa ninajaribu ku—kutafuta jinsi ya kulitenda; sikujua jinsi ya kuomba. Niliweka mikono yangu, kisha nikalala hivi. Bila shaka, Shetani alijitokeza wakati huo, kasema, “Unaona? Umengojea mda mrefu mno. Umekwisha fikia miaka ishirini, hakuna haja ya kujaribu hilo sasa. Umeisha. . .”

Ndipo nikavunjika moyo na kuanza kulia. Ndiposa, nilipokuwa nimevunjika moyo kabisa, nikasema, “Nitazungumza. Kama hunizungumzii, nitakuzungumzia hata hivyo.” Kwa hivyo na—nalisema, “Sifai kitu; najionea aibu! Bwana Mungu, najua utanisikia mahali fulani. Unanisikia? Najionea aibu; naona aibu kwamba sikukujali.”

Mnamo wakati huo nilitazama juu, na kitu cha kuisimua kilipita mwilini mwangu. Hapa ikaja Nuru ikipitia mle chumbani na kufanya msalaba, hivyo; na Sauti ambayo sijawahi kusikia maishani mwangu, ikanena. Nikaitazama, nimekuwa baridi mwili mzima, nikifa ganzi; tokana na hofu. Singeweza kusogea. Nikasimama, niliingalia; na ikaenda zake.

Nikasema, “Bwana, mimi—mimi sielewi lugha Yako.” Nikasema, “Kama huwezi kuzungumza yangu, na mimi—na mimi sielewi Yako. . . Na kama umenisamehe, najua kwamba ninapaswa kuhesabiwa katika msalaba ule pale, mahali ambapo—dhambi zangu zinapaswa kuwekwa mle. Na kama—na kama utanisamehe, rudi na uzungumze katika lugha Yako. Nitajua kwa hiyo, kama huwezi kuzungumza lugha Yangu.” Nikasema, “Hebu irudi tena.”

Ndiyo hiyo hapo tena. Lo, jamani! Hapo nikapata Yakini. Amina! Naam, bwana! Nilijisikia kana kwamba m—mzigo wa tani arobaini uliondolewa mabegani mwangu. Nilitembea nikishuka kupitia ubao ule, sikuweza kugusa ardhi.

Mama alisema, “Billy una mwamsho wa niva.”

Nilisema, “La, mama, sijui kile kilichotendeka.”

Palikuwa na njia ya reli pale; niliteremka mbio nikifuata njia hiyo ya reli nikiruka juu hewani kwa nguvu nilivyoweza. Sikujua jinsi ya kujieleza jinsi nilivyojisikia. Lo, kama ningejua jinsi ya kupaza sauti! Nilikuwa nikipaza sauti, lakini kwa njia yangu mwenyewe. Unaona?

Ilikuwa ni nini? Niliweka nanga nafsi yangu katika Kituo cha Salama. Hilo lilimaliza kila kitu; hiyo ilikuwa Yakini yangu. Hapo nilikuwa nimepata kitu fulani, si hadithi fulani, wazo fulani. Nilikuwa nimezungumza na Mtu yule. Nilikuwa nimezungumza na yule Mtu aliyeniambia nisinnye pombe kamwe, au kuvuta sigara, au kufanya kitu cho chote ambacho kingenichafua—na wanawake na kadhalika; kwamba nitakapokuwa mtu mkubwa kungekuwa na kazi nitakayofanya. Nilikuwa nimewasiliana naye, si kanisa; nilikwisha wasiliana Naye—Yeye! Naam, bwana! Alikuwa Ndiye.

Kama mtu fulani hapa kwenye Kiwanis au ile—alikuwa akizungumza si mda mrefu. Mara baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia (Ndugu Funk akisimama pale, akiwa askari)—alisema kwamba alikuwa . . . (Ni mdogo—yasikika namna fulani ya utani. Si mahali pa utani; lakini hili ndilo alilosema. Alikuwa hapa New Albany.) Alisema, “Kapiteni alitupeleka nje, akasema, ‘Nchi yote pale imezungukwa na Wajapani. Kesho, enyi Vijana, tutaingia, hatuna budi kuwateka.’ Alisema, ‘Kumbukeni, enyi Vijana, kuna wengi wetu wasimamao hapa leo ambao hawatakuwepo kesho. Hawatakuwepo hapa kesho; tunaingia, kesho asubuhi kwenye mapambazuko.’ Kasema, ‘Sasa kila mmoja wenu aende kwenye dini yake?’”

Jamaa huyu akasema, “Na mimi sikuwa na dini yo yote.” Kisha akasema, “Nikasema . . .” Kasema, “Nilisimama hapo na watu wengine wote . . .” Kasema, “Hapa yuaja kasisi, akaenda upande *huu*; Mprotestanti akaenda upande *huu*, na Myahudi akaenda upande *huu*, na Mkatoliki akaenda upande *ule* pamoja na kasisi wao.” Kasema, “Nilisimama pale.”

Kisha kasema, “Yule—yule afisa mwenye amri aliniambia, akasema, ‘Kijana, afadhali uende kwenye dini yako.’”

Alisema, “Sina yo yote.”

Akasema, “Afadhali ukipatie dini fulani, sababu utahitaji baadhi yake punde si punde; nina hakika.”

Na akasema mnamo wakati ule, aliona kundi moja likipita na lilikuwa la Wakatoliki. Kasema alikwenda akamwambia kasisi huyo, “Weweza kunipa dini kidogo?”

Naye akasema, “Njoo!”

Akasema, “Aliingia na kunifanya Mkatoliki.” (Na hapo New Albany walikuweco John Howard na kundi la hao

Wakatoliki waaminifu wakikaa hapo, wajua, wakati jamaa huyu alipokuwa akielezea hili.) Naye alisema—alisema, “Siku iliyofuata kwenye vita...” Alikuwa akizungumzia kuhusu, lo, jinsi ilivyokuwa na alisema (yeye ni mtu mkubwa mno, wajua)—na alisema walipambana ana kwa ana. Nao walikuwa tu wakichomana visu, na kupiga makelele, na kukatana na kuchinjana. Kasema mistari ilipindika kisha wakazungukana. Wajapani waliwaachilia waingie ndani, hivyo, na hizo bombom kubwa za kale zilinguruma pande zote—mapambano ya ana kwa ana.

Kasema, “Moja kwa moja, nilisimama kirefu *hivi*...” Kisha kasema “Kila kitu, kupiga makelele na kuendelea na vurugu, usingeweza kujisikia.” Kasema, “Kuna damu.” Akasema, “Niliangalia, nayo ilikuwa ni damu yangu!” Kasema, “Nikatazama *hapa*. Palikuwa na tundu ubavuni mwangu.” Kasema, “Hiyo ilikuwa damu yangu.” Kasema, “Mimi... Wajua, mimi... mimi... mimi...”

Na wakweli... Na rafiki Mkatoliki, nasema hili kwa—kwa kutufurahisha sasa. Lakini Mkatoliki halisi na mwaminifu, akasema—akasema, “Je, ulisema ‘Salamu Maria?’”

Akasema, “La, bwana!” Akasema, “Hiyo ilikuwa damu *yangu*. Sikutaka makatibu wo wote. Nilisema, ‘Nataka kuzungumza na Bwana mkubwa.’” Kasema, “Hiyo ilikuwa—hiyo ilikuwa damu yangu.”

Nami nafikiri hivyo ndivyo ilivyo. Ndiyo, bwana! Hivyo ndivyo ilivyo. Yatubidi tuwe na nguzo ya kushikilia, Yakini.

“Sikuwa na wakati wa katibu Wake,” alisema, “Nalitaka nizungumze Naye.”

Na ndivyo ilivyo, ndugu. Mtu ajapo kwa Kristo, hautaki kuchukua neno la mhubiri fulani, neno la katibu fulani, kitu fulani kingine. Ninyi Waprotestanti, msichukue *hili*, *lile*, au *lile lingine*, nendeni kwenye ile Yakini mpaka mtakapotia nanga hapo kwa kuzaliwa upya, mkizaliwa mara ya pili na kujazwa Roho Mtakatifu, na kuona Biblia ikidhihirishwa katika unyenyekevu na upendo katika maisha yako. Lo, basi hiyo ndiyo Yakini yako. Ndiyo, bwana!

Nilisoma katika Neno ambapo Yeye ni Neno. Kanisa la Kijerumani liliposema, “Ni *njia hii*,” na la Kimethodisti na la Kibaptisti na la Kikatoliki... Lakini nilisoma katika Neno, ambapo Yeye alisema, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda.”

Sikiliza sasa, katika kufunga. Sasa, Mprotestanti asema... Sasa Mkatoliki husema alilijenga juu ya Petro. “Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu...” La, hakujenga kamwe! Kama ingekuwa hivyo, lilirudi nyuma moja kwa moja. Walilijenga juu ya mwanadamu. Alifanya nini?

Waprotestanti walisema alilijenga juu ya Yake Mwenyewe. La! Hakufanya hivyo! Hakulijenga juu ya Yake Mwenyewe. Alifanyaje?

“Watu hu—Watu hunena Mimi, Mwana wa Adamu, ni nani?”

Na baadhi yao walisema, “Wewe ni Eliya, na Musa”

Alisema, “Lakini *ninyi* mwasema nini?”

Petro akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu Aliye Hai.”

Angalia yale maneno sasa. “Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona; nyama na damu havikukufunulia hili (hakujifunza hilo kwa kasi fulani; hakujifunza hili katika seminari), lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia. Na juu ya mwamba huu (ufunuo wa kiroho wa Neno), nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

Nikawaza, “Bwana ndiyo hiyo.” Nilisoma hapa katika Kitabu cha Ufunuo sura ya 21—sura ya 22, ambapo alisema, “Ye yote (hili ndilo jambo timilifu)—ye yote atakayeingiza kitu fulani katika Hilo; mtu ye yote atakayeondoa kitu fulani kutoka Hilo (kukana ndivyo lilivyo) au ye yote atakayejaribu kulifanya zuri zaidi, kuling’arisha kwa ajili ya siku hizi; ye yote atakayeliongeza au kuliondoa, yuyo huyo ataondolewa, sehemu yake, katika Kitabu cha Uzima.”

Nikasema, “Basi hayo ndiyo tu yote ninayohitaji, Bwana, ni kuamini *Hili*. Na katika *hili*, msalaba ule kule, Kristo alikuja.” Ni kamilifu wakati wote, kila neno ambalo Yeye amewahi ku sema. Chukua kitabu katika mkono *huu*, na historia katika mkono *huu*, na inadhihirisha sawa wakati wote, kamili tu. Nami nilisema, “Basi Bwana, nipokee!” Na nilipofanya hayo, nilimpokea Kristo, Roho Mtakatifu, moyoni mwangu, Yakini yangu. Haijakuwa eti ni mimi.

Nilikuwa mgonjwa wakati mmoja wakati ni—nilipompoteza mke wangu; nilimpoteza mtoto wangu mchanga; lo, nilimpoteza baba yangu, na nilimpoteza ndugu yangu, na nilimpoteza shemeji yangu. Na Billy alikuwa analala, akifa, na—na nilikuwa mahututi sana. . . Nilikuwa nikienda zangu barabarani nikilia, nikienda kwenye kaburi lake (naye na yule mtoto mchanga, huku amemshika huyo mtoto)—nikienda kaburini. Nilikuwa nikitembea huko juu; Bw. Isler (alikuwa akiya hapa kucheza) mnajua Mbunge wa mkoa wa Indiana), alikuwa akienda zake barabarani. Alisimama akikimbia kule na kunikumbatia (ilikuwa baada ya mafuriko ya 37); akasema, “Unakwenda wapi, Billy? Juu kule?”

Nami nikasema, “Naam!”

Akasema, “Unaenda kufanya nini huko juu?”

Nikasema, “Ninamsikiliza hua wa kale.” Nalisema, “Mimi huketi kule kwenye kaburi la mtoto na lake. Hua wa kale huja pale, naye hunizungumzia.”

“Lo,” akasema, “Billy!”

Nikasema, “Ndio! Nasikia mnong’ono wa majani wanapoucheza. Hunichezea muziki.”

Bw. Isler alisema, “Yanacheza muziki wa aina gani?”

Nikasema,

Kuna nchi kule ngambo ya mto
Ambayo wao huiita tamu siku zote,
Nasi twafika tu ufuko huo kwa agizo la imani;
Mmoja mmoja twaingia langoni,
Hapo kuishi na wasiokufa.
Wakati siku moja watapiga hizo kengele za
dhahabu kwa ajili yako wewe na mimi.

Akasema, “Billy, nataka kukuuliza jambo fulani.” Akasema, “Je, Kristo anamaanisha nini kwako sasa? Kristo anamaanisha nini kwako?”

Nikasema, “Yeye ni Uzima wangu, kila Kitu. Yeye ni kila kitu nilicho nacho, Bwana Isler. Yeye ni Uamuzi wa—wangu wa Mwisho; Yu kila kitu ambacho naweza kukishikilia.”

Kwa nini? Kungelitokea jambo fulani.

Juu ya mwamba huu . . .

Akasema, “Nimekuona ukisimama hapa pembeni ukahubiri mpaka ulionekana kana kwamba ungeanguka ufe. Nimekuona saa zote za usiku huku na huko barabarani ukiwashughulikia wagonjwa. Na baada ya Yeye kuchukua mkeo na mtoto wako mchanga, bado unamtumikia?”

Nikasema, “Kama akiniva, bado namtumaini.”

Kwa nini? Nanga yangu hushikilia humo bondeni; nikiwa na Yakini. Nimejifunga kwa Neno Lake, nalo Neno Lake lilikuwa likishikilia. Yeye ndiye Yakini yangu. Nimeona kwamba vitu hivi vingine vyote vyaweza kushindwa, lakini Kristo kamwe hashindwi.

Kanisa Katoliki lina papa kama yakini, Waprotestanti wana maaskofu, na kanuni zao za imani, na waangalizi wao, lakini mimi, kama Paulo . . .

Una penseli yako? Andika jambo fulani! Katika . . . Paulo alisema katika Matendo sura ya 20 na aya ya 24, “Lakini hakuna mojawapo ya mambo haya hunitikisa mimi.”

Lo, waweza kuwa na kanuni za imani; waweza kuwa na lo lote unalotaka kuwa nalo, lakini hayo hayanitikisi mimi!

Nimetia nanga nafsi yangu katika kituo cha
 salama,
 Kuabiri bahari zilizochafuka (sijui upo wapi,
 upande huu, upande ule) tena;
 Tufani yaweza kupita juu ya vilindi
 vilivyochafuka, (wote waweza kukataa)
 Lakini katika Yesu ni salama zaidi.

Naam! hakuna mojawapo ya mambo haya, hunitikisa mimi,
 kwa kuwa nimefungiliwa kwenye Nanga.

“Lo, tangu nilipokutana Naye,” Paulo alisema, “barabarani
 mle, nimekwishafungiliwa kwenye Nanga. Alinigeuza;
 alinirudisha nyuma vema.” Unakumbuka, Paulo alikuwa mtu
 wa dhehebu pia (kubwa zaidi ya yote nchini), lakini alifungiliwa
 kwenye ile Yakini.

Sikilizeni! Nataka niwaambie kitu. Alikuwa na kusudi
 katika kuniokoa; alikuwa na kusudi katika kukuokoa. Nami
 nimeamua, kwa mapenzi Yake, kulifanya, si kuliongeza au
 kulipunguza (Ufunuo 22:19, kama ukitaka kuandika hilo).
 Sawa! Ye yote aondoaye... Nimeamua (Ninakaribia kuliacha
 kanisa, nanyi mwajua hilo), na kwa hiyo nimeamua kudumu na
 Injili kadiri niwapo hai kwa msaada wa Mungu.

Kumbuka! Hapa pana neema. Kulikuwa na mamilioni
 wakifa katika dhambi aliponiokoa. Mimi nilikuwa nani
 kwamba angeniokoa? Alikuwa na kusudi katika kuniokoa,
 nami nimeamua kutekeleza kusudi hilo. Sijali; labda mwisho
 wangu waweza kuwa karibu sana sasa, lakini hata iwe nini, bado
 nimetia nanga. Sijaibadilisha kamwe.

Bw. Isler akaniambia siku ile, akitembea barabarani;
 akasema, “Billy, katika matatizo haya yote ulishikilia dini
 yako?”

Nikasema, “La, bwana, ilinishikilia.” Unaona, unaona?
 Nanga yangu ilishikilia. Sikuishikilia kamwe, ilinishikilia.
 Siwezi kuishikilia; haiwezekani kamwe kufanya hivyo, lakini
 inanishikilia. Hivyo tu.

Alikuwa na kusudi katika kuniokoa. Kulikuwa na mamilioni
 katika dhambi nilipomjia, lakini aliniokoa. Alikuwa na kusudi
 katika kufanya hivyo. Kifo cha Kristo kilikuwa Yakini kwa
 hofu yake.

Kifo cha Kristo kilimaliza lile swala. Wakati nyuki yule wa
 mauti alipomuuma na kumchoma ule mwiba... Mwajua, nyuki—
 mdudu ambaye ana mwiba; kama akiwahi kuchoma mwiba
 kwenye—ndani vya kutosha, wakati anapouvuta, ule mwiba
 unamtoka. Mauti siku zote imekuwa na mwiba.

Mauti siku zote ilikuwa na mwiba, na siku moja wakati
 huo—akienda Kalvari, na kugongana-gongana na miamba, damu
 ikimwagika na kuruka juu ya miamba... Ilipogonga takataka

hapo Kalvari, akienda Golgotha, sehemu ya nyuma ya msalaba ule ilikuwa ikifuta alama za nyayo zenye damu za ule maskini mwili dhaifu uliokuwa ukienda, ukijongea kule (wao wakimpiga na kumpondaponda alipokuwa akipanda kile kilima); lakini alikuwa na Yakini. Alijua aliposimama, kwa sababu Neno la Mungu lilisema kupitia Daudi, “Sitamuacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu; wala sitaiacha nafsi yake kuzimu.”

Alijua uharibifu huanza katika masaa sabini na mawili; alisema, “Livunjeni hekalu hili, nami nitaliinua tena katika siku tatu.” Alikuwa na Yakini!

Hapo yuapanda kile kilima na huku akizomewa kwa dhihaka, mate ya askari waliolewa, ambao waliweka tambara chafu usoni Mwake, wakampiga kichwani, na kusema, “Wewe ni nabii, tuambie nani kakupiga!” Huyu hapo yuaenda juu kilimani katika aibu na fedheha apate—nguo Zake zimevuliwa, akidharau aibu, akining’inia juu ya msalaba mbele ya watu, uchi wa mnyama; akifa katika aibu ya Kirumi chini ya adhabu ya serikali ya kifo, Mtu ambaye hakufanya kitu cho chote.

Hadithi ndogo wakati mmoja ilisemekana Mariamu Magdalena alitoka mbio na akasema, “Amefanya nini? Kaponya wagonjwa wenu, kafufua wafu, na kuwaletea wokovu wale ambao—kifungoni. Amefanya nini?”

Kisha kasisi akampiga kofi la mdomoni, mpaka damu ikaruka na kububujika, akasema, “Utamsikiliza yeye au kuhani wako mkuu?” Lo, ulimwengu ule wa kidhehebu; ni laana ya kila kitu. Hivyo tu. Ndiyo hiyo.

Nao wakamchukua. Lakini alipokuwa akipanda kilima akikokota... Ibilisi alikuwa siku zote akilitilia shaka, Yeye kuwa kile alichokuwa. Kasema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, geuza mawe haya yawe mkate. Unadai unaweza kufanya miujiza. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yageuzwe yawe mkate.”

Ibilisi huyo huyo wa kale anaishi sasa. Hilo ni kweli. “Kama wewe ni mponyaji wa Kiungu, hapa yupo mzee Yohana *fulani* ameketi hapa pembeni; najua ni kiwete; mponye!” Hamjui ni ibilisi yule yule wa kale?

Yesu alisema, “Natenda tu...” Angalia! Alipitia katika kisima cha Bethsaida, ambapo maelfu walilala pale, viwete, vipofu, vilema, na waliopooza, akamwendea mtu aliyeweza kutembea. Aliweza kwenda huku na huko; huenda alikuwa na shida za kuvunjika nguvu. Hata iwe nini, alikuwa haendelei (ameugua yapata miaka thelathini na minane). Akasema, “Kila ninapokuja birikani, mtu mwingine hushuka mbele yangu.” Aliweza kutembea. Aliwaacha wote wamelala pale, akamwendea huyo hasa, akamponya. Kwa nini?

Alisema alijua alikuwa katika hali ile. Ndipo wakamwambia, walimswali walipomuona (Yohana Mt. 5);

akasema, “Amini, amini nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda...” Hiyo ndiyo Yakini Yake. Hiyo bado ndiyo Yakini.

Nikisimama kule Finland siku ile, na yule mvulana mdogo akiwa amelala pale, nami nilimzunguka akiwa amelala pale amekufa (alikuwa amekufa kwa nusu saa. Mlisoma katika kile kitabu)... Nilianza kuondoka; kitu kiliweka mikono yao juu. Nikageuka; nikawazia, “Hicho kilikuwa nini?” Nikaangalia tena. Nikafikiri, “Ngoja dakika mmoja!” Nikaangalia nyuma hapa katika karatasi ya kwanza ya Biblia, “Na itakuwa, mvulana mdogo mwenye umri wa kama miaka tisa... Atauwawa na gari. Kutakuwa kipande kirefu cha nchi yenye miti isiokauka, mawe yamerundikana hapo; gari hilo litakuwa limekingama barabarani, limeharibika kabisa. Atakuwa amevaa soksi ndefu kama—zimevutwa juu, nywele zake zimekatwa; na vijicho vyake vitakuwa vimeguezwa nyuma, mifupa katika mwili wake itakuwa imevunjika.”

Nikaangalia; nikawazia, “Ee, Mungu!”

Nikasema, “Simameni kimya ninyi nyote!” (Meya wa mji akiwepo.) Nikasema, “Kama mvulana yule hasimami kwa miguu yake katika muda wa dakika mbili tangu sasa, mimi ni nabii wa uwongo. Nifukuzeni mnitoe Finland.” Hakika! “Lakini kama akisimama, yatoeni maisha yenu kwa Kristo.” Hilo ni kweli. Walisimama kimya.

Nikasema, “Baba wa Mbinguni, kule ng’ambo, miaka miwili iliyopita, ulisema mvulana huyu mdogo atalala hapa...”

Hapa palikuwepo na Ndugu Moore na Ndugu Lindsay, na wao wakiliangalia hilo. Na kila mahali, nao walikuwa wameliandika katika Biblia; na maelfu ya Biblia nchini mwote zilikuwa na hilo limeandikwa mle. Ilikuwa nini? Yakini.

Baba alikuwa ameonyesha ambalo litatokea. Hakuna hofu kamwe kusimama pale—Yakini. Hakika, atainuka.

Huko huko Finland, ambapo maelfu ya watu walikuja kila usiku (na ilibidi hata kuwatoa wengine nje na kuwaacha wawe—kuwakalisha; kuwatoa na kumwingiza mtu mwingine ndani), huyo hapo amesimama pamoja na... Wote wale—hao watu walionipenda; nao walikuwa wameona uponyaji ukifanyika; lakini hapa palikuwa na mvulana aliyelala pale amekufa. Yakini ilikuwa nini? Lile ono. “Natenda ambalo Baba husema nitende. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Ndiyo hiyo hapo Yakini yako.

Nikasema, “Mauti, huwezi kumshikilia tena; Mungu amenena! Rudi; mwachilie!” Na yule mvulana mdogo aliinuka akaangalia pande zote hivyo; watu wakaanza kuzimia na kila kitu.

Ndilo hilo, limeandikwa hapo na kutiwa sahihi na meya wa mji, na karani wa hati za sheria. Hilo ni kweli! Ni nini? Yakini. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama huyo si Mungu yule yule ambaye alimsimamisha mwanamke yule toka Naini na—huku amembeba mwanawe wa kiume.

Mtu ye yote alipokufa siku hizo, mara moja walimweka kaburini; hawakuwaacha wakae, waliwaweka kaburini. Hapo yupo Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Naam!

Angalia chini kule Mexico wakati mtoto yule mchanga (baadhi yenu mlio hapa—mnaoketi hapa), na mtoto yule (daktari alitia sahihi maandishi; imeandikwa katika Wafanyi Biashara Wakristo), mtoto yule mchanga alikuwa amekufa asubuhi ile saa tatu, na hii ilikuwa saa nne usiku. Na maskini mama yule hakukubali kufarijiwa. Billy akisimama pale, mwanangu, akijaribu kumrudisha, na alikuwa... Vema, wao, nabuni, walikuwa na walinzi mia mbili wamesimama pale; naye alipanda juu yao. Usiku uliotangulia, yule kipofu alipata kuona; naye alijua. (Alikuwa Mkatoliki.) Lakini hatimaye, nilisema, “Nenda, Ndugu Moore, ukamwombee, kwa sababu mtoto yule mchanga...” Ilikuwa inanyesha, ikinyesha kwa nguvu, walikuwa wamesimama pale tangu mapambazuko (nje katika uwanja wa michezo ya dume). Nami nikasema... Niliteremshwa kwa kamba kule nyuma niweze kufika mahali hapo, nilikuwa pale kwa siku tatu usiku.) Nilisimama pale, nikasema, “Nilipokuwa nikinena...” (kuhubiri) kisha nikaangalia; niliona mtoto mchanga nje hapa mbele yangu, mtoto mchanga wa Kimexico, hana meno, akiwa ameketi tu pale, alinichekea—papa hapa mbele yangu. Nikasema, “Ngoja kidogo, ndugu Moore, mlete huyu mama hapa.” Lo, Yakini!

Wale walinzi walipisha njia; ndiye huyu anakuja. Alianguka chini akasema, “Padri, Padri!”

Nikasema, “Simama!”

Na ndugu Espinoza akasema, “Simama (na alimuambia katika Kihispaniola).” Akasimama hapo.

Nikasema, “Baba wa Mbinguni, ninasimama hapa katika mvua hii...”

Mama mzuri mdogo wa miaka kama ishirini na mitatu, kitu kama hicho, nywele zake zikining’inia chini, uso wake mdogo ukiangalia juu hivyo, mtazamo wa macho yake—matumaini; alikuwa amemuona yule mtu aliyekuwa kipofu kabisa kwa yapata miaka arobaini, macho yake yalifunguka jukwaani. Alijua ikiwa Mungu aliweza kufungua macho yaliyopofushwa, angeweza kumponya mtoto wake mchanga. Ndiye huyo amelala hapo, kitu kidogo kigumu kimelala chini ya blanketi hivyo, kimelowa maji. Alikuwa amesimama hapo asubuhi nzima na mchana huo pia. Alikuwa hapo mnamo saa tano—saa nne usiku ule, kitu kama hicho, akimshikilia mtoto yule mchanga

(mmeona maelezo yake katika Wafanyi Biashara Wakristo) hapo, akimshikilia mtoto yule hivyo.

Nikasema, “Baba wa Mbinguni, sijui hili linamaanisha nini. Mimi ni mtumishi Wako tu, lakini nilimwona mtoto huyo mchanga akisimama kule; alikuwa hai. Naiweka mikono yangu juu yake katika Jina la Bwana Yesu.

Kasema, “Waa!” Akaanza kulia. Mama yake akamnyakua na kuanza kulia kwa nguvu, na watu wakaanza kulia kwa nguvu kila mahali, na wanawake wakizimia, na kadhalika. Nikasema, “Msiseme kitu juu yake. Pelekeni mtu akimbie na mtoto huyo—na mama huyo, mwende kwa yule daktari, na hebu na aweke sahihi maandishi kwamba huyo mtoto alikufa. Alikufa kwa ugonjwa wa pafu asubuhi iliyotangulia na—au asubuhi hiyo saa tatu.” Nasi tunayo maandishi yaliyotiwa sahihi na daktari, mtoto yule alitangazwa kwamba amekufa katika ofisi ya daktari asubuhi hiyo, na mama yule naye akambeba siku nzima. Ilikuwa nini? Yakini!

Ilikuwa nini? Aliamini kwamba kama Mungu angeweza kufungua macho yaliyopofushwa, kwani, Mungu angeweza kuwafufua wafu; kwani ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Sikuwa na hakika; sikujua mpaka nilipoona. Na nilipomuona yule mtoto, ilikuwa Yakini. Sawa sawa kabisa! Ndiyo hiyo. Kifo kilipaswa kitoe mfu wake.

Hapa akatoka Mwana wa Mungu; nyuki yule wa mauti akaanza kumvumia. “Hasha, angeweza kuwa nabii! Angeweza kusimama pale na kuacha—kudemewa mate usoni Mwake? Angeweza kusimama pale na kuwaacha wamdhihaki na asifanye kitu! Huyu si Imanueli! Huyu ni mtu tu wa kawaida. Angalia hayo mate ya pombe toka kwa hao askari waliolewa. Angalia uso Wake ukitoka damu!”

Ibilisi alisema, “Nitampata. Nitampata.” Huyu hapa yuaja kama nyuki, mwiba wa mauti, akimvumia. Lakini, ndugu, wakati nyuki huyo alipomchoma kwa mwiba Imanueli, alipotoka, alipoteza mwiba wake, hata kifo chenyewe.

Si ajabu Paulo baadaye aliweza kukiangalia usoni na kusema, “Ee mauti, uwapi uchungu wako; kaburi, ku wapi kushinda kwako? Mungu na ashukuriwe atupaye ushindi.” Kifo cha Kristo kilikuwa Yakini kwa kila mtu ambaye alikiogopa.

Moyo wangu unasema “amina” kwa kila neno katika Kitabu Chake. (Ninafunga, bila shaka sasa. Inanibidi tu kulikatiza hili. Unaona?

Ndiyo maana najua kwamba Roho Mtakatifu ni Dira yangu ambayo huniongoza. Ni yeye anayenifanya nijue Neno hili ni kweli; Yeye ndiye Yakini yangu; Yeye ndiye Jua langu; Yeye ndiye Uzima wangu; Yeye ndiye Nanga yangu! Matatizo yanapozuka, Yeye ndiye Nyota yangu ya Kaskazini.

Ninapopotea, Roho Mtakatifu ndiye Dira yangu inayoniongoza kunirudisha mahali pale.

Madhehebu ni kama nyota zingine; husogea pamoja na ulimwengu. Nyota zingine husogea jinsi ulimwengu unavyosogea, lakini si Nyota ya Kaskazini. Ulimwengu unaweza kusogea mahali unapopenda, lakini hiyo haisogei kamwe. Lo, jamani! Nyota ya Kaskazini imetia nanga. Zingine husogea hapa na pale; waweza kuzionga hapa na pale, na kila mahali. Hivyo ndivyo ilivyo kwa makanisa ya kidhehebu. Lakini Kristo ndiye ile Yakini. Ndiye unayeweza kumtumainia. Madhehebu yanapowasonga ninyi nyote, angalieni tu Nyota ya Kaskazini. Roho Mtakatifu ndiye Dira yenu.

Yeye daima hudumu wakweli kwa Neno Lake. Waliponiambia kwamba mambo hayo hayawezi kutokea katika siku za kisasa kama hizi, nilijua kama—kama—kama hakuna Mungu, basi ishi, kula, kunywa, na ufurahi. Kama kuna Mungu, hebu na tumtumikie Yeye. Nami nimeishi kuiona siku ile ambapo ametenda kila kitu, hata kuwafufua wafu alipokuwa hapa duniani. Nasi twajua hayo kwa maandishi yaliyoandikwa kwamba ni kweli. Ndio, bwana! Yeye ni Yakini yangu.

Sasa, mfanye Yeye Yakini yako. Chukua katika—nyakati za shida zangu, Yeye siku zote ndiye Yakini yangu. Sasa angalia, kwa neema ya Mungu. . . (Sasa, afadhali nifunge. Muda umeendelea sana. Vema, angalia hapa, nilifikiri ilikuwa saa tano; na ni 6:30.)

Marafiki, siku nzima, usiku wote, mwaka wote, na katika Milele yote kamwe singeweza kulinena. Usijaribu kuliwazia. Huwezi. Hakuna njia ya kuliwazia. Unasema, “Ndugu Branham, kama—kama wewe. . .”

Mimi sijui; ninaamini tu; ninaacha kujaribu kufanya kitu cho chote kuhusu hili; ninaliamini tu. Hayo tu. Unaona? “Si yeye apigaye mbio, wala yeye atakaye, Mungu ndiye arehemuye.” Unaona? Si kwa matendo, ni kwa neema. Unaona? Ninaliamini tu. Mungu ni. . . Ni juu Yake kutenda yale mengine. Liamini tu. Tenda linavyosema.

Wimbo huu ujulikanao sana, niliwasikia wakiucheza—wakiuimba hapa au mahali fulani:

Lo, upendo wa Mungu, jinsi ulivyo tajiri na
halisi!
Jinsi usivyo na kina na ulivyo na nguvu!
Siku zote utadumu,
. . . wimbo wa watakatifu pamoja na malaika.

Wakati mtu kwa hesabu alijaribu kuvunja-vunja, au alipojaribu kuonyesha kwa elimu yake, itakutia wenda wazimu. Huwezi kulifanya. Usijaribu kulifanya. Usijaribu kuliwazia; Mungu hawezi kuwaziwa. Humuwazii Mungu, unamwamini Mungu tu. Hilo ni—hiyo ndiyo siri. Usiliwazie, amini tu.

Siwezi kukumbuka maana yake; siwezi kukwambia namna ya kulifanya. Ninajua tu, ninaliamini tu; Hayo tu.

Kama tu, unamwahidi mtoto mdogo kitu fulani, anaamini hilo. Yakupasa utimize neno lako. Wewe ni mtoto wa Mungu. Yeye hutimiza Neno Lake; kwa unyofu tu liamini. Usitikiswe; kaa tu papo hapo. Mungu alilitenda wakati mmoja, hana budi kulitenda tena. Kama halitendi, atakwambia kwa nini hawezi kulifanya. Na hilo ni kweli. Sasa, kaa tu nalo.

Mwajua, aya hiyo mmoja pale... Naamini ndugu yetu wa thamani pale (alibatizwa usiku uliopita) anaimba wimbo huo, *Lo, upendo wa Mungu*. Wananiambia kwamba hiyo aya, sehemu hii yake, ilikuwa imeandikwa kwenye ukuta wa hospitali ya wenda wazimu, iliposema:

Kama tukiijaza bahari kwa wino,
 Au kama mbingu zingalitengenezwa kwa
 karatasi za ngozi;
 Na kila kikonyo duniani kiwe unyoya wa
 kuandika,
 Na kila mtu awe mwandishi.
 Kuandika upendo wa Mungu aliye juu
 Itakausha bahari,
 Au gombo lingalitoshwa kila kitu,
 Hata likitandazwa toka mbingu hadi mbingu.

Fikiria hilo, wakati ambapo robo tatu ya dunia ni maji. Na angalia hewa ya haidrojeni, na oksijeni hewani, unyevu na kadhalika. Unaona? Kama kila unyevu ungekuwa wino, basi fikiria mabilioni, na matrilioni na matrilioni ya mirija ambayo ingekuwa kalamu za unyoya. Na fikiria mabilioni ya watu ambao wamekuwa duniani na kila mmoja wao kazi yake iwe ni mwandishi. Kuchovya hizo kalamu za wino baharini na kujaribu kuwazia upendo wa Mungu kutakausha bahari, au kama gombo lingaliingia kila kitu, hata likitandazwa toka Milele hata Milele.

Usiuwazie jinsi ulivyo; huwezi. Utarukwa na akili ukijaribu kuuwazia; amini tu. Mfanye Yakini yako! Kaa hapo; amani tamu na ujuzi ambao hutausahau kamwe, tia nanga hapo, na nanga yako itashikilia bondeni. Na tuinamishe vichwa vyetu.

Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Jinsi Wewe ulivyo mkuu! Ni wangapi wenu ndani hapa huku vichwa vyenu vikiwa vimeinamishwa asubuhi hii... Inakaribia mwaka mpya sasa; nanyi mmekuwa wa kidini sasa (na hivyo ni vyema, ninapenda hilo, kila mmoja wenu. Nina hakika Mungu anapenda hilo), lakini kwa kweli hujapata tukio hilo la Yakini, kitu ambacho hukuamini kwa kujifanya tu, hukukiwazia tu akilini, lakini kitu fulani kilinena nawe. Kisha uliona maisha yako yakibadilika tangu wakati huo, na kila Neno la Mungu, kila ahadi unaiitikia na "Amina." Basi unashikilia kwenye ile Yakini, sababu unakumbuka, yeye alisema, "Mbingu na nchi zitapita, lakini

Neno Langu halitashindwa.” Hujafikia mahali hapo bado ambapo ungeweza kusema “Amina” kwa kila Neno, kama ingekuwa kinyume cha kanuni zako za imani, ilikuwa kinyume cha dhehebu lako, lakini unataka kufikia mahali pale kama Musa, kama wengine wao (ambao hawakuweza kufanya hilo mpaka waliposhika ile Yakini), nawe waihitaji katika maisha yako asubuhi hii, hebu onyesheni vivyo hivyo kwa kumwinulia tu Mungu mikono yenu. Mungu awabariki. Sawa, bwana. Kila mahali hapa ni kukutumikia Wewe.

Baba wa neema, najua kwamba wakati mwingine lazima tuachane. Hapana budi kuna wakati basi tutakapouacha ulimwengu huu. Hatujui hilo litakuwa wakati gani, na haijalishi sana. Kama muda wetu umeisha, basi tunataka kuja. Kusudi letu la kukaa hapa ni kukutumikia Wewe.

Na tangu kuwa katika njia iendayo kwenye uharibifu siku moja, kama Paulo alivyokuwa njiani akielekea Dameski kuliudhi Kanisa, Nuru ilimpofusha. Na ee, Mungu, hiyo Nuru ilimfuata, kwani ilikuwa Kristo. Naye alitia nanga hapo kwenye Yakini kwamba hata kifo chenyewe, angeweza kucheka mbele yake, na kusema, “Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Yesu Kristo.”

Ulikuwa Yakini kamilifu kwa Mtume yule. Alikuwa ile—ulikuwa ile Amina kwake katika kila sentensi. Ulikuwa Nyota ya maisha yake, nguzo ya Kuongozea. Wewe ulikuwa Dira ambayo ilimuongoza katika tufani. Ulikuwa ndiwe Ufunuo; Ulikuwa ndiwe Ono lile; Ulikuwa Matumaini yake, Wokovu wake. Na hata wakati wa kufa kwake, alipojua anauendea, Wewe bado ulikuwa ndiwe Yakini yake.

Wewe ulikuwa Yakini ya Danieli. Ulikuwa Yakini ya manabii wote. Katikati ya tofauti za kidhehebu, na matatizo ya wakati wao, na Mafarisayo na Masadukayo, bado kulikuwa na watu ambao walikuchukua Wewe kama Yakini yao.

Na leo, Bwana, wanaume na wanawake kwa huruma, kwa upendo na—na mioyo ambayo inatoka damu, Bwana, kwa tukio la kweli la kumjua Mungu, na kuwa na—uhakika wa yakini, labda yote watu waliowahi kujua hapo mbeleni, Bwana, ilikuwa kujiunga na kanisa. Nasi twatambua, kama nilivyojaribu kwa unyofu wa moyo, si kuwa tofauti (unajua moyo wangu), lakini kuwaambia huwezi kujiunga na lile Kanisa, unajiunga na chumba cha kulala, Methodisti, na Batisti, na Katoliki, na vyumba vya kulala vya Kipentekoste; lakini unazaliwa katika Kanisa—Mwili wa kisiri wa Kristo, na kuwa washirika wa Mwili Wake, na vipawa vya Roho kuufanya Mwili Wake mkuu uingie kazini na uwezo.

Mungu, hilo ndilo ambalo mikono hii ilimaanisha asubuhi hii iliponyoshwa. “Niweke, ee Bwana. Nichukue, nifinyange, nitengeneze, ifanye tu sehemu yangu katika maisha Yakini sana,

nikifungiwa kwa Kristo hivi kwamba sitafikiria kitu kingine ila hiyo Yakini.” Tujalie, Bwana. Wabariki. Waponye wagonjwa na wanaoteseke. Waokoe waliopotea.

Sasa, Bwana, twajua ni kawaida kuwaita watu madhabahuni, lakini hilo limekuwa desturi kwetu. Na asubuhi hii huku madhabahu yamejaa na hao—na hao watoto wadogo na—na wote... Lakini, Bwana, kwa namna fulani Wewe ulizungumza nao; waliinyosha mikono yao. Walifanya—walifanya, kana kwamba ilikuwa uamuzi. Wanataka kufanya hivyo, wao—wao—wao wanataka kitu halisi, na ninatoa maombi yangu kwa niaba yao. Mjalie kila mmoja, Bwana.

Uwe pamoja nasi sasa, ukitusamehe dhambi zetu, ukiponya maradhi yetu, na ukitupa ukombozi tunaohitaji.

Na, Bwana, juu ya mambo yote, hebu na tusingahau leo kwamba tumefungwa kwenye ile Yakini, Nyota yetu ya Kaskazini, kwenye Kalvari, kwa Kristo, na Roho Mtakatifu anachukua maneno ya Mungu na kuyadhihirisha waziwazi kwetu kwa kuponya wagonjwa, akituonyesha maono, akifufua wafu, na akitenda sawa kabisa na yale aliyoahidi kufanya.

Na naomba kanisa hili na watu hawa, wa sehemu ya Mwili wa Kristo ambao wamekusanyika hapa asubuhi hii, waishi kama Yesu alivyosema waishi: “Ninyi ni chumvi ya dunia.” Na naomba wakolee, mpaka jamii zao waone kiu. Chumvi huleta kiu, na chumvi yaweza tu kuokoa inapogusana na kitu. Nami naomba, Mungu, kwamba utatoa hili kwa watu, wapate kuwa wanaowapata watu.

Mbariki mchungaji wetu, Ndugu Neville, huyu mtumishi mnyenyekevu, Bwana, akisimama kwenye sehemu yake ya kazi akiwa mwenye uchaji, kama mshiriki wa Mwili wa Kristo, akijaribu kwa jitihada zake zote kufuata kila kitu ambacho ungemwambia atende.

Wabariki wadhamini, hao watu waliosimama nami vizuri sana katika wakati huu mkuu wa giza ambao nimeupitia. Walisimama pamoja na Kanisa, hao walioomba nami na kusimama nami katika nyakati za taabu. Bwana, ninawapenda, nami natoa maombi yangu kwamba watakutegemea Wewe, Bwana. Na waondoe matumaini yao katika udongo huu upatikanao na mauti wa mtumishi; na wamwangelie Yeye, ambaye ni Mwenye Nguvu zote, ambaye ni... Nasi tunajua, Bwana, kwamba sisi tuna kikomo. Haidhuru sisi ni akina nani, bado tu watu wafao. Lakini si mjumbe, bali Ujumbe. Tujalie, Bwana. Hapo ndipo ambapo tunaelekeza kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Tujalie kwamba atakuwa halisi sasa kwa kila mmoja wetu hapa leo, hata kwa watoto wadogo, kwamba atakuwa ndiye Yakini ya kusanyiko nzima. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari

Sasa, tunapouimba tena, salimiana kwa mikono na mtu aliye mbele yako, nyuma yako, karibu nawe; kila mtu na asalimiane kwa mikono sasa. Endeleeeni kuketi; geukeni mkasalimiane kwa mikono mkiweza. Mnaona?

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Wametangaza hivi sasa usiku wa Jumatatu Ushirika kwenye usiku wa manane. Hebu tuinue mikono yetu sasa na tumwimbie. Ni wangapi—wangapi mnajisikia—Yeye ni Yakini yenu? Neno, Yeye ni Neno. Unaamini hilo? Yeye ni Neno, na Roho Mtakatifu amehuisia Neno lile kuifanya Nuru hiyo iishi ndani yako, ya Neno, udhihirisho wa Neno. Weka Neno lile katika moyo wako; acha Roho Mtakatifu aingie, kisha liangalie Neno lile likifanya kazi. Amini, kuwa mnyenyekevu; usitamani kuwa mtu fulani mkuu; usiwe kitu, ili Mungu apate kukufanya mtu wa maana. Unaona? Sawa. Fanya hivyo sasa.

Kila mmoja anayempenda aseme, “Amina!” [Kusanyiko linaitikia “Amina!”—Mh.] Mnajua neno *Amina* linamaanisha nini? “Na iwe hivyo.” Amina! Sawa.

Natuseme, “Haleluya!” [Kusanyiko linajibu,

“Haleluya!”—Mh.] Mnajua maana yake? “Bwana asifiwe!”

Nilipokuwa Ujerumani si muda mrefu uliopita, nilisimama mbele ya watu kama thelathini au arobaini elfu nje kule siku hiyo, nami nalisema, “Ni ajabu kwamba ninyi Wajerumani hamwezi mkaelewa.” Nikasema, “Nilipokuwa nikija huko leo, mbwa alinibwekea kwa Kiingereza.” Hiyo ni kweli. Nilisema, “Hakuwa na taabu hata. Na hapo alikuwepo ndege, naye akaniambia katika Kiingereza. Nilishuka nikaja barabarani na mama fulani alikuwa na mtoto mchanga mkononi mwake, nilipoingilia nyuma kule huko nyuma.” Kisha nikasema, “Mtoto yule mchanga alikuwa analia katika Kiingereza. Mna nini enyi watu?” Hilo ni kweli. Lo, kama ukiangalia tu pande zote, Yeye yuko kila mahali, sivyo? Hakika yupo.

Sasa, hebu na tuinue mikono yetu tu, na kufumba macho yetu, na kuimba, tunapomuomba mchungaji aje aturuhusu tuondoke. Hebu na tusimame kwanza. Kila mtu asimame. Kila mtu, mnampenda, tena sasa? Semeni, “Amina!” Nanyi mnajua, neno *Haleluya* ni neno lile lile katika kila lugha? Nenda kwenye misitu ya Wahotentoti huko Afrika; *Haleluya* ni neno lile lile. Haleluya! Linapaswa kabisa kuwa salamu za Kikristo, sivyo? Haleluya! Neno lenyewe humaanisha “asifiwe Mungu wetu.”

Naye anastahili hilo, sivyo? Hakika Yeye ni Mwokozi wangu, yeye hakika ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwangu mimi. Hakika ni yeye yule jana, leo, na hata milele kwangu. Yuko namna hiyo kwako?

Nampenda, nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.



YAKINI SWA62-1230M
(Absolute)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, Desemba 30, 1962, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1989 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org